CHUO CHA BIBLIA

# VITABU VYA
# MATENDO YA MITUME NA WARUMI

KITABU CHA 12

## Sura Ya Kwanza

## ‘Matendo Ya Kristo Aliyefufuka’

Kitabu cha Matendo ndicho Cha kipekee cha historia ya Kanisa ambacho kimevuviwa katika Agano Jipya. Kinaunganisha Injili nne pamoja na nyaraka kumi na tatu za Paulo. Kama sio kwa kitabu hiki cha historia, wakati ungeanza kusoma nyaraka za Paulo, ungejiuliza, ‘ni nani huyu anayetajwa kama mtume Paulo? Mimi si msomi hata kidogo wa vitabu vya Injili.’ Kutakuwepo na kiunganishi kikubwa ambacho kitakosekana katika Agano Jipya bila kitabu hiki ambacho tunataka kukikagua sasa.

Kuna hali ambapo vitabu vya kwanza tano vya Agano Jipya ni vya historia. Hali kwamba Injili ni historia ya maisha na matendo ya Yesu iliyovuviwa, na pia ni vitabu vya historia. Hata hivyo, kitabu cha Matendo kimetengwa kutoka kwa Injili kwa sababu ni cha historia ya Kanisa la Agano Jipya.

Kitabu cha Matendo kinaanza hivi: *‘Kitabu kile cha kwanza nilikiandika, Theofilo, katika habari ya mambo yote aliyoanza Yesu kufanya na kufundisha, hata siku ile alipochukuliwa juu, alipokuwa amekwisha kuwaagiza kwa Roho Mtakatifu wale mitume aliowachagua* (Matendo 1:1,2).’

Kutokana na mistari hii ya kwanza ya kitabu cha Matendo, tunafahamu kwamba mwandishi wa kitabu hiki ndiye yule yule ambaye aliandika kitabu cha Injili ya Luka, na kwamba kitabu hiki anakielekeza kwake mtu yule yule ambaye alimwelekezea Injili ya tatu. Theofilo, ambaye jina lake linamaanisha ‘mpenda Mungu,’ ambaye yaonekana alikuwa mtu ambaye Luka alimkisia kuwa anastahili kupokea hati hizi mbili muhimu sana.

Katika kitabu cha Matendo, Luka anaendelea na hadithi ile ambayo alianzia katika Injili ambayo inatajwa kwa jina lake. Luka anaandika kwamba, katika Injili yake, alikuwa ametupatia habari sahihi za kihistoria kuhusu yale yote Yesu aliyotenda hadi kupaa mbinguni. Hata hivyo, Luka anatupasha kwamba, baada ya kupaa mbinguni, Yesu aliendelea, ‘kutenda na kufunza’ kupitia mitume. Hivyo basi, tafsiri nyingi za Biblia zinataja kitabu hiki, ‘Matendo ya Mitume.’

Tunapofahamu umuhimu wa Siku ya Pentekoste, tunaamini kwamba jina bora kwa kitabu hiki yawezekana kuwa ni, ‘Matendo ya Roho Mtakatifu kupitia mitume.’ Kwa kuwa Petro anataja

ishara na maajabu ya Pentekoste kuwa ya Kristo aliyefufuka na kuishi, kwa hakika, jina bora lingekuwa, 'Matendo ya Kristo aliyefufuka kupitia mitume (2:32, 33).'

Hebu tambua kwamba kitabu cha Matendo hakifiki mwisho – kinakatwa mara moja tu. Baadhi ya wasomi wanaamini kwamba, hii ilikuwa kwa sababu Luka alishikwa na hivyo basi, hangeweza kumaliza kitabu hiki. Wengine wanaamini kwamba kitabu hiki hakina mwisho kwa sababu ni historia ya Kanisa, nasi tungali tukiandika historia hiyo.

## Cha Kutazamia Katika Kitabu Cha Matendo

Kwa kuwa kitabu cha Matendo ni cha historia, unahitajika kukikaribia jinsi ulivyotenda katika vitabu vile kumi na viwili vya historia katika Agano la Kale. Paulo aliandika hivi kuhusu historia ya Waebrania: 'Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mfano, yakaandikwa hili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani (1 Wakorintho 10:11).' Tafuta mifano na onyo wakati unaposoma kitabu hiki.

## Kusudi La Kanisa

Unaposoma kitabu hiki cha historia, tazama kusudi ambalo lilipewa Kanisa. Wakati Yesu alipofika mwisho wa wakati wake kuwa pamoja na mitume, Aliwapa 'Agizo Kuu.' Utapata Agizo Kuu hapo mwisho mwa kila Injili. Kulingana na Mathayo, haya yalikuwa maneno ya mwisho ya Yesu kwa wanafunzi wake:

'*Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana,na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari* (Mathayo 28:18-20).'

Kitabu cha historia cha Agano Jipya kinaanzia kwa njia ile ile ambayo Injili zile zingine nne zinamalizia, kwa Agizo Kuu. Agizo hii Kuu kwa hakika lina jukumu moja tu – 'kuwafanya wanafunzi.' Kisha kuna kanuni nne ambazo zinafafanua jukumu hili – kuwafanya wanafunzi: Kwenda, Kuhubiri, Kubatiza na Kufunza.

Katika kitabu hiki cha Matendo, haya ndiyo kwa hakika yaliyotokea. Mitume wanafanya wanafunzi kwa Kwenda, Kuhubiri, Kuwabatiza na Kuwafunza. Kusudi ambalo limepewa Kanisa,

kuanzia mwanzo ni Agizo Kuu. Agizo Kuu ndio hati kuu (kusudi lililonakiliwa) la Kanisa.' Kama mashirika yale mengine, ni lazima Kanisa litimize masharti ya hati yake au lididimie na kutoweka.

## Ahadi Iliyotolewa Kwa Kanisa

Katika mistari ya kwanza ya kitabu hiki, tunaambiwa, kwamba kabla ya kupaa mbinguni, Yesu aliwapa mitume wake amri. Pamoja na Agizo Kuu, Yesu alikuwa amewapa amri kwamba wangoje. '*Ngojeeni ahadi yake Baba itimiziwe* (Matendo 1:4,5).' Yesu alikuwa amewahidi huko katika chumba cha orofani kwamba angelimtuma Roho Mtakatifu kwao. Naye hapa anawapa amri kwamba wasichukue hatua ye yote kutii Agizo ile Kuu hadi wakati ahadi ile itakapotimizwa.'

Maandiko yana mengi kuzungumzia kuhusu kumngojea Bwana. Isaya aliuhubiri mojawapo ya mahubiri nayapendayo kuhusu kule kungojea: *'Bali wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia* (Isaya 40:31).'

Wakati Isaya alipowaambia watu wa Mungu, kungojea jinsi tai angojeavyo, alikuwa akishiriki kweli yenye thamani kuu kuhusu imani. Kuna wakati tai hawapai. Wakati tai anapoiona tufani ikikaribia, yeye huketi ukingoni mwa kiota chake kwa muda mrefu sana, yamkini kwa masaa kadhaa, na kungoja hadi wakati tufani hilo linafanyika kuwa na wimbi lenye kasi kuu. Hapo ndipo tai huyo huruka juu kwa kimo cha takribani mita kama tano, juu ya wimbi lile lenye mwendo wa kasi na kuzifungua mbawa zake maridadi na kupokea uwezo unaohitajika kumwinua juu zaidi ya wimbi na tufani ile.

Unaposoma sura ya kwanza ya kitabu cha Matendo, lifananishe na Kanisa na yule tai ambaye anaketi kando mwa kiota chake, akingojea wimbi la Roho ambalo litakuja katika Siku ya Pentekoste. Unaposoma sura ya pili ya kitabu hiki, hebu mfikirie yule tai akiruka kutoka kwa kiota chake, huku akitumainia kuwa lile wimbi litampatia uwezo wa kuruka na kuwa juu ya uovu ambao atakumbana nao.

## Uwezo Uliopewa Kanisa

Sura ya pili inaeleza kuja kwa Roho Mtakatifu Siku ya Pentekoste. Hili ni tukio moja muhimu katika historia ya watu wa Mungu, kwa sababu kwa hakika, Kanisa haliwezi kutimiza kusudi lake, ikiwa uwezo wa Roho Mtakatifu hauko juu yake. Hii pia ni kweli katika maisha mwaminifu binafsi.

Tunapojaribu kufanya mwanafunzi kwa ajili ya Yesu Kristo, huwa tunajaribu kitu ambacho hakiwezekani kutendeka bila uwezo wa Roho Mtakatifu.

## Utendaji Wa Kanisa

Yamkini unakumbuka kwamba mafunzo ya Yesu mlimani hayakuwa kuhusu kuhitimu, bali utendaji (Mathayo 5-7). Kulingana na Yesu, jambo lenye umuhimu mkuu sio lile ambalo tunanena, bali tunalotenda. Anatilia mkazo thamani hii wakati alipowafunza mitume. Hatuhitaji kushangaa wakati tunaposoma kwamba ulimwengu wa karne ya kwanza ulishangazwa na matendo ya Kanisa.

Kuna mambo mengi ambayo unahitajika kutambua kuhusu matendo ya Kanisa. Kwanza, unahitaji kutazama mahubiri ya mitume. Kuna mahubiri makuu ambayo yamenakiliwa katika kitabu hiki cha historia, na kwamba mahubiri hayo yanaanzia siku ya Pentekoste. Matokeo muhimu katika Pentekoste yalikuwa kwamba, kulifanyika wanafunzi elfu tatu kupitia mahubiri ya Petro huku maelfu wakiokolewa kila mara Petro alipohubiri kuifuatia siku ya Pentekoste.

Mahubiri ya mitume katika kitabu cha Matendo ni mahubiri yaliyovuviwa. Hili inamaanisha kwamba Roho wa Mungu aliwajia walipokuwa wakihubiri. Hili linatajwa kama ‘upako’ katika Biblia ambao maanake ni kutiwa nguvu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu juu ya yule anayehubiri au kuhudumu kwa karama za Roho.

Kwa umakinifu mkuu, hebu tilia maanani mahubiri ya Petro yalionakiliwa katika kitabu cha Matendo. Kwa hakika, hakuna cho chote ambacho kinaonekana kuwa maalumu kuhusu mahubiri hayo. Hivyo basi, ni kwa sababu gani maelfu ya watu walipata kuokolewa baada ya mahubiri ya Petro? Kulikuwepo matokeo yasiyo ya kawaida kwa sababu Petro alikuwa na upako wa Roho Mtakatifu alipohubiri. Wanafunzi wa Yesu walishtakiwa kwa kujaza mji wa Yerusalemu kwa mafundisho yao (5:28). Je! Wafuasi wa Yesu wa siku ya leo, tuna mashtaka kama haya? Na je! Kuna ushahidi wo wote wa kutushtaki ikiwa ingekuwa hivyo?

## Hivyo Basi, Kanisa Ni Nini?

Unaposoma kitabu cha Matendo, tia maanani kwamba unajulishwa kwa takribani watu hamsini kwenye kitabu hiki cha historia ya Kanisa la Agano Jipya. Neno ‘Kanisa’ kwa lugha ya Kiyunani ni ‘*Ecclesia’* maanake makutano’ au ‘wale walioitwa nje.’ Hii inamaanisha, ‘makutano ya

watu ambao wameitwa kutoka ulimwenguni hili kumfuata Kristo aliyefufuka na anayeishi, na kuwa na ushirika pamoja naye, na pamoja na watu wengine.' Kwa hivyo, maana kamili ya 'Kanisa' ni 'watu.'

Unaposoma kitabu hiki kwa mara ya kwanza, jaribu kujifahamisha kwa karibu watu hamsini wakiwepo Petro na Paulo. Kitabu cha Matendo ni historia ya watu wa kawaida wakitenda mambo yasiyo ya kawaida kwa kuwa wao walikuwa wamevuviwa na kujazwa na Roho Mtakatifu wa Mungu. Mungu yule yule pamoja na uwezo Wake kwa ajili yako na mimi hili kutenda kazi yake siku ya leo (Mathayo 28: 18-20).

Unapomtumikia Mungu siku ya leo, je! Wamjia kabla ya kwenda? Je! Wamngonjea katika uwepo Wake hili akupe upako na kukutia nguvu za Roho Mtakatifu, au unaenda na kujaribu kutenda kazi Yake kwa uweza wako mwenyewe? Mojawapo ya jumbe za Kitabu hiki ni kwamba, bila usaidizi wa Mungu, hatuwezi kuitekeleza kazi Yake. Hivyo basi, ni lazima tungojee uwezo wa Roho Mtakatifu kabla ya kujaribu kutenda kazi ya Kristo aliyefufuka.

## Sura ya Pili

## 'Alama Za Vidole Zinazoonekana Za Kanisa Lisiloonekana'

Sura ya pili inaanza kwa kuelezea siku ya Pentekoste ambayo ilikuwa ndio siku ya kuzaliwa kwa Kanisa (Matendo 2:1-18). Tunaposoma sura hiyo ya pili, ni muhimu ikiwa tutatambua kwamba siku ya Pentekoste ilikuwa siku kuu ya Kiyahudi. Hii ilikuwa siku ya sherehe za mavuno, 'Siku Ya Kumtolea Mungu Shukrani' wakati Wayahudi walipomshukuru Mungu kwa mavuno yao. Kuna mfano na mafumbo makuu hapa. Hii ni kwa sababu ya mavuno makuu ya kiroho yaliyokuwa yamekaribia kutokea siku hiyo. Katika siku ya Pentekoste, Kristo aliyefufuka alianza kujenga Kanisa ambalo lingefanya uinjilisti kote ulimwenguni pamoja kwa ajili yake.

Hii iliwezekana kwa sababu Roho Mtakatifu alishuka chini kwa uweza mkuu siku ile. Kulikuwepo na ishara na maajabu ambayo yalifuatana na kuja kwa Roho Mtakatifu. Kulikuwepo na sauti kama ya upepo mkuu wenye kuvuma. Ndimi kama za moto zilizogawanyika zilikaa juu ya vichwa vyao wale ambao walikuwa 'wakitabiri.' Kisha watu 'wakanena kwa lugha nyingine.'

Swali na jibu linatusaidia kutilia mkazo maana ya tukio hili la kimiujiza. Swali lile lilikuwa hili: 'Maana yake ni nini?' Petro alijibu swali hili katika ujumbe wake: 'Hili ndilo lile ambalo lilitabiriwa naye

nabii Yoeli.' Yoeli alikuwa ametabiri kwamba, katika siku zile za mwisho, Mungu angemwaga Roho wake juu ya wana wake wa kiume na wa kike nao wangetabiri (Yoeli 2:28,29).

Katika siku ya Pentekoste, ujumbe ambao uliotokana na muijiza wa ndimi ni 'unabii', au ujumbe kutoka kwa Mungu ambao unaelekezwa kwa masikio ya watu.

Paulo anaanidika kuhusu muijiza ambao anautaja kama 'karama au kipawa cha ndimi.' Anataja kwa uwazi mwingi kwamba karama hii ya ndimi ambayo anaizungumzia ni tofauti na zile ndimi ambazo zilinenwa siku ya Pentekoste. Aliandika kuwa, *'Maana yeye anenaye kwa lugha, hasemi na watu, bali husema na Mungu; maana hakuna asikiaye; lakini anena mambo ya siri katika roho yake* (1 Wakorintho 14:2).'

Wakati muumini anapotekeleza karama hii ya ndimi, ujumbe wake hauelekezwi kwa masikio ya wanadamu. Yeye anazungumza na Mungu. Yeye hazungumzi na wanadamu, jinsi wale wanenaji walivyotenda siku ya Pentekoste. Huwa ananena na Mungu. Lakini lugha au ndimi ambazo tunasoma kuhusu katika siku ya Pentekoste zilikuwa zikiwasiliana kuhusu unabii, ujumbe kutoka kwa Mungu kwake mwanadamu. Ndimi hizo zilikuwa mojawapo ya miujiza na ishara nyingi ambazo zilifuatana na kuja kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste.

Kuna zaidi ya Pentekoste moja ambazo zimenakiliwa katika kitabu cha Matendo. Kwanza, kuna Pentekoste ya Yerusalemu. Pia kuna nyakati mitume walienda huko Samaria na nyakati kadhaa wanapovuka hadi kwa watu wasio Wayahudi, na kushuhudia Pentekoste. Tambua kwamba, kila wakati kunapokuwa na sherehe za Pentekoste, inahusu sababu ilitolewa kwa Kanisa katika Agizo Kuu: *'Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi* (Matendo 1:8).'

## 'Alama Za Vidole'

Kuna jambo moja ambalo unafaa kutambua unaposoma kitabu cha Matendo. Tambua taratibu ambazo zinaibuka katika kizazi cha kwanza cha Kanisa. Kwanza kabisa, tambua taratibu au mfumo wa Kanisa lenyewe. Waweza kutaja mfumo huu kama 'alama za vidole zinazoonekana za Kanisa lisiloonekana.' Wasomi huzungumzia kuhusu Kanisa linaloonekana na lisiloonekana,' au Kanisa la ulimwengu na Kanisa linalodhihirika katika maeneo fulani. Ushirika wa waaminifu ambao

wewe ni sehemu yao katika jamii iliyopo eneo lako, na dhihirisho la Kanisa lililositirika na la ulimwengu wote la Kristo aliyefufuka, ambalo analijenga katika ulimwengu huu.

Je! Tunaweza vipi kufahamu kwamba Kanisa la eneo letu ni dhihirisho lililositirika, na la ulimwengu kote? Jinsi alama za vidole vyetu vinaweza kututambulisha pahala tulikuwepo na kile tulichogusa, Kanisa linaweza kutambulishwa kwa 'alama za vidole.' Hebu tazama 'alama za vidole' unaposoma kuhusu Kanisa la kizazi cha kwanza. Kanisa katika kitabu cha Matendo lilikuwa na 'alama za vidole', dhihirisho lisilositirika la kweli na la ulimwengu wote.

Uinjilisti ulikuwa 'alama ya kidole cha gumba' cha Kanisa ambalo lilizaliwa siku ya Pentekoste. Mitume walifahamu kwamba walihitajika kwenda kote kama wamishionari na wainjilisti. Watu elfu tatu waliokolewa katika siku ya Pentekoste, na maelfu wakaokolewa baadaye wakati mitume na wengine walipohubiri Injili.

Mafunzo yalikuwa 'alama ya kidole cha shahada' cha Kanisa. Tunasoma kwamba wale waongofu wapya waliendelea katika mafunzo na ushirika, katika kuumega mkate, na katika maombi pamoja na mitume (Mitume 2:42).'

'Kidole cha kati' kisichositirika cha Kanisa lililositirika kilikuwa ushirika. Mitume waliamini kwamba watu wale ambao waliwafunza walihitaji kushirikiana nao. Neno la Kiyunani kwa 'ushirika' ni ''koinonia.' Neno hili linamaanisha kuwa katika ushirika ambao misingi yake ipo katika maagano yenye kujitolea. Maagano na kujitolea kwa wale waaminifu katika kizazi cha kwanza kulikuwa kwa Yeye aliyefufuka, Kristo anayeishi kwanza, kisha kati yao.

Hawa mitume walitoa wapi dhana hii kwamba wale waliokuwa wakifunzwa walihitajika kushirikiana na wale waliokuwa wakiwafunza? Unaweza kukumbuka kutoka uchambuzi wetu wa Injili ya Yohana kwamba wakati baadhi yao walipokutana na Yesu, walimwuliza kuwaonyesha pale alipoishi (Yohana 1:37-39). Yesu aliwajibu kwa kuwakaribisha kuja na kuona pale alimoishi, nao wakaishi pamoja naye, na kufa kwa ajili Yake kwa sababu ya yale waliyoshuhudia wakati walipojitolea kwenda kwake. Waliiishi pamoja naye kwa miaka mitatu. Hii ndio sababu hatuhitajiki kushangaa wakati tunaposoma na kutambua kwamba watu wale waliookoka siku ya Pentekoste walikuwa na thamani maalumu ya ushirika na wale waliowafanya kuwa wanafunzi.

‘Alama ya kidole cha pete’ ilikuwa kuabudu. Tunasoma kwamba wale waongofu walikuwa wamejitolea ‘kuumega mkate’ pamoja na mitume (Matendo 2:42). Hii ilimaanisha Meza ya Bwana au Ushirika Mtakatifu. Wakati Yesu alipozindua ‘Meza ya Bwana’, na kuwaagiza kushiriki katika meza hiyo hadi atakaporudi (1 Wakorintho 11:26), alikuwa akiwapa mitume mafunzo yake mwenyewe jinsi alitaka Kanisa lake kuabudu (Luka 22:14-19). Na hivyo wakati wanafunzi wa kwanza walipokutanika pamoja, waliabudu kwa kushiriki katika Meza ya Bwana.

Pia tunasoma kwamba walidumu katika maombi na mitume – ‘vidole vidogo’ visivyositirika vya Kanisa lililositirika. Kwa sababu hatuwezi kutenda kazi ya Kristo aliyefufuka pasipo kuwa ndani yake, ni lazima tuendelee kuomba na kuchukua uwezo kutoka mzabibu wa kiroho wa Kristo aliyefufuka (Yohana 15:1-16). Yesu alikuwa amewafunza mitume kudumu katika maombi na kwa uvumilivu, kuomba, kutafuta, na kubisha kwa sababu, kila atendaye hivyo, hupokea na kupata kisha milango hufunguliwa naye Mungu Baba huwapa Roho Mtakatifu (Luka 11:9-13; Mathayo 7:7-11).

‘Yuko Wapi Yeye?’

Agano Jipya linaanza kwa maswali ya wale mamajusi watatu wakiuliza, ‘*Yuko Wapi Yeye?* (Mathayo 2:2).’ Yesu alituambia kwamba atalijenga Kanisa lake nazo nguvu za kuzimu hazitaweza kumzuia (Mathayo 16:18). Mtume Yohana ananakili ufunuo usio wa kawaida wa Kristo aliyefufuka na kutembea kati ya Makanisa ya (Ufunuo 1:13-2:1). Ufunuo huo unajibu swali la wale mamajusi: Yuko wapi yeye ‘miongoni mwa’ Makanisa. Hapo ndipo Yeye yupo na kile anachotenda siku ya leo. Alianza ile kazi ya miujiza katika kitabu cha Matendo na u ngali anafanya hivyo hata siku ya leo.

Je! Tunaweza kutumia kipimo kipi cha afya, au kupokea ‘ishara muhimu’ kutoka kwa Makanisa yetu siku ya leo? Kwanza kabisa, twahitajika kutazama ushahidi wa alama za vidole. Tunapoziona alama hizi za vidole katika Makanisa yetu, kwa kile kipimo cha moja hadi kumi, twahitajika wakati wote kuhudumia Kanisa zetu kwa: Uinjilisti, mafunzo, ushirika, ibada na maombi, nasi tutaona jinsi yanavyolingana na Kanisa la kizazi cha kwanza ambalo tunalipata katika kitabu cha Matendo.

Hivyo basi, tutakuwa na kiwango cha vipimo ambavyo twaweza kutumia hili kutuwezesha kusema kwamba Kanisa letu ni dhihirisho lisilositirika la Yesu Kristo aliyefufuka analolijenga katika ulimwengu wa leo.

## Sura Ya Tatu

## 'Mfumo Usiositirika Wa Kanisa Lililositirika'

Haikuchukua muda mrefu baadaye Kanisa la Agano Jipya likakumbana na vitisho na changa moto mbali mbali. Jinsi tunavyotazama viongozi wa Kanisa wakikumbana na matatizo hayo, – dhiki kutoka nje na matatizo miongoni mwao– mifumo fulani unaibuka. Mifumo hii ni baadhi ya mifano na yale maonyo ambayo Paulo alikuwa ametuambia kwamba yalihitajika katika kutufunza na kutuonya siku ya leo wakati tunaposoma historia ya Biblia (1 Wakorintho 10:11).

Kwa mfano, mfumo wa kutoa unazinduliwa mapema katika historia ya Kanisa. Tunasoma kwamba wale waliokuwa na mali waliuza na kuleta mapokeo yao kwa mitume hili kugawiwa kulingana na mahitaji ya waaminifu. Wao walitoa zaidi ya kile kiwango cha fungu la kumi, au matoleo yo yote; walitoa kila kitu walichokuwa nacho.

Pia tunaona jinsi ya kuasi katika jamii. Huu ni mfumo wa ajabu. Yesu alisema*, 'mlipeni Kaisari yaliyo ya kaisari, na Mungu yaliyo ya Mungu* (Mathayo 22:21).' Mungu hakuuliza kile kilichokuwa cha Kaisari, lakini kuna wakati Kaisari atauliza kilicho cha Mungu. Wakati Kaisari anapouliza kilicho cha Mungu, mfano huu wa Agano Jipya unatuambia kwamba hatuwezi kumpa kile kilicho cha Mungu.

Mitume waliamrishwa na Yesu kuhubiri na kufunza jina na Injili ya Yesu Kristo. Lakini viongozi wa dini na wale wa kijamii waliwaamrisha kutolizungumzia jina la Yesu kwa mara nyingine (Matendo 4:18). Mara ya kwanza jambo hili lilipotokea, wao kama watu walio wa kawaida, hawakuwa wamehitimu kusema kwamba ilikuwa vema kumsikiliza Mungu au viongozi. Baadaye, wao walikuwa na mkutano wa maombi. Wakati mwingine wale viongozi walipowakataza kulihubiri jina na Injili ya Kristo, walijibu bila kusita, *'ni lazima tumtii Mungu kuliko kumtii mwanadamu!* (Matendo 5:29).' Na huu ni uasi wa kijamii! *(Civil disobedience).*

Kuna nyakati kulingana na mwito wa wafuasi wa Kristo, ni lazima wateseke kwa kuwa ni matokeo ya kumtii Mungu na Kristo, kuliko kumtii mwanadamu. Kote kati ulimwengu na vizazi vyote hata siku ya leo, waaminifu wanateswa sana. Waaminifu wengi wamefariki kwa ajili ya imani yao tangu miaka ya 1940 hadi vita vya pili vya dunia, kuliko katika historia yote ya Kanisa.

Pia tunaona mfumo wa nidhamu Kanisani ukiibuka. Kulikuwa na mtu aliyejulikana kama Anania na mkewe Safira ambao waliuza shamba lao. Wao walisema uongo kwa mitume kuhusu jumla ya mapato ya fedha walizopokea kutoka kwa malipo ya shamba lao. Katika hadithi hii, Petro alidhihirisha ufafanuzi wa kushangaza. Aliwauliza hivi, '*mbona mmefanya hila hili kusema uongo kwake Roho mtakatifu!* (Matendo 5: 3,4).' Wakati walipokaripiwa kila mmoja peke yake kuhusu dhambi yao, walikufa!

Nidhamu hii ya Kanisa ililifanya kuwa lenye utakaso na kutia hofu ya utakatifu ya kumcha Mungu miongoni mwa wanafunzi. Nao watu wa ulimwengu huko Yerusalemu walifahamu kwamba ilikuwa jambo la kutiliwa umuhimu mkuu kufikiria kufanyika mfuasi wa Kristo na kuwa mshirika wa Kanisa (Matendo 5:11-13).

Katika Matendo sura ya sita, kuna mfumo ambao unaibuka ambao unahitajika kutumiwa wakati Kanisa linapokua. Kanisa lilikuwa likikua kwa haraka mno, likiwa na watu wengi wakiishi pamoja kwa hali ya kijamii. Wakati maelfu ya watu wanapoishi pamoja ambao wahitajika kulishwa mara kadhaa kwa siku moja, ni lazima kuwe na utaratibu wa chakula (6:1). Mitume walijipata wakivutwa katika usimamizi wa mradi au utaratibu ule, na wajibu huu uliwavuta mbali na huduma yao ya Neno la Mungu. Hivyo basi, mitume waliita mkutano wa waaminifu wote na kusema: *'Wale thenashara wakawaita jamii ya wanafunzi, wakasema, Haipendezi sisi kuliacha Neno la Mungu na kuhudumu mezani. Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kijawa na Roho, na hekima, hili tuwaweke juu ya jambo hili; na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumu lile Neno* (6:2-4).'

Wakati hili lilipotendwa, waliwaamuru wale waliokuwa wamechaguliwa kusimamia jukumu hili hali wao wakajitolea kabisa kwa maombi na huduma ya Neno la Mungu. Uamuzi huu ulibarikiwa sana na Mungu, na matokeo yake yalikuwa ni kuenea kwa Injili katika mji wa Yerusalemu. Huu ndio mwanzo wa wale ambao wafahamika kama mashemasi. Ulikuwa wajibu wa mashemasi waliochaguliwa kusimamia huduma hiyo ya Kanisani hili watu wenye karama au vipawa vya uchungaji wawe huru kujitolea kwa huduma ya uchungaji.

Utangulizi huu uliowekwa na Kanisa wakati huu ulikuwa kudhibitisha zile kanuni kwamba kuna fursa katika mwili wa Kristo kwa kila mwanafunzi. Watu wote wenye upako, wenye kutia nguvu

kutoka kwa Roho Mtakatifu wana vipawa vya kiroho. Baadhi ya vipawa hivyo ni vya uchungaji ilhali vingine vya kiroho na utendaji.

Vipawa vya utendaji, ambavyo Agano Jipya linavitaja kama ‘usaidizi’, au ‘serikali au utawala’, au ‘uongozi’, ni vya kiroho sawa na vya mtu anayehubiri, kufunza, au kueneza Injili. Hata hivyo, kila mwanafunzi ahitajika kusimama mahali pake na kutumia kipawa chake ambacho Mungu amempa. Kanisa ambalo hupokea na kutumia mfumo huu hubarikiwa na kukuzwa.

Je! Wewe umegundua mfumo wa kipawa chako cha kiroho? Punde utakafanya hivyo, jitolee kikamilifu kwa huduma ambazo kipawa chako kinakuwezesha kutenda kwa ajili ya Bwana. Mfumo huu huhuzisha mwanafunzi ambaye amethibitika kuwa mwaminifu katika matendo, na baadaye kuvuka hadi huduma ya uchungaji. Stefano aliyekufa kwa ajili ya Kristo pamoja na Filipo aliyekuwa mwinjilisti ni mifano wa mfumo huu wa uvukaji kutoka walimokuwepo kama mashemasi waaminifu kisha baadaye kufanyika wainjilisti.

Mfumo mwingine ambao unaibuka katika kitabu cha Matendo ni wa kufa kwa ajili ya Injili. Msemo unaotambulikana kutoka historia ya Kanisa ni: *‘Damu yao watakatifu walioifia Injili ndio mbegu ambayo hulifanya Kanisa kukua.’* Stefano alitoa maisha yake kwa ajili ya mahubiri yake (7:54-60). Wakati Stefano alipokufa kwa ajili ya imani yake, mtu aitwae Sauli wa Tarso alikuwa ameshikilia mavazi ya wale waliokuwa wakimpiga kwa mawe. Inawezekana kuwa kuokoka kwa Sauli kulitokana na ushawishi kutoka kwa kifo cha Stefano. Hili ndio maana ya msemo huu kuhusu damu ya watakatifu kukuza Kanisa.

Mfumo mwingine ulio dhahiri na wa kuvutia katika Kanisa ni uponyaji. Kuna kutiliwa mkaza juu ya uponyaji katika historia ya Luka kuhusu Kanisa jinsi ilivyokuwa kulingana na Injili yake. Kulingana naye, Yesu aliyefufuka kwa wakati huu anatenda kazi kupitia mitume hili kuendeleza huduma ya uponyaji.

Petro na Yohana walikutana naye aliyeketi kwenye lango la Hekalu. Alikuwa mwenye umri wa miaka arobaini na mwenye kilema. Maisha yake yote, alikuwa akimbebwa na mtu hadi langoni mwa Hekalu ambapo alikuwa akiomba usaidizi. Wakati Petro na Yohana walipokuwa wakienda Hekaluni, yule mtu alikuwa hapo akiwa na kombe lake. Petro akasema, ‘*Mimi sina fedha, wala*

*dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho nikupacho. Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama uende! (*3:6).'

Tunasoma kwamba yule mtu hakusimama tu na kutembea. Aliingia ndani Hekaluni akiruka-ruka na kumsifu Mungu! Kiongozi mmoja wa dini mwenye kiburi amenukuliwa hivi karibuni akisema, '*Kanisa haliwezi tena kusema, Fedha na dhahabu hatuna.'* Naye akajibiwa na mtumishi mwingine wa Bwana kuwa, *'Nalo Kanisa haliwezi kusema, Katika jina la Yesu Kristo wa Nazareti, tembea!*'

Uponyaji huu, kama huo wa Yesu kwa yule mtu aliyekuwa kando ya birika la Bethsaida (Yohana 5), unawapa mitume fursa kuu ya kuhubiri Injili. Viongozi wa kiroho walishangaa wakati walipowaona wavuvi hawa ambao hawakuwa wenye elimu wakihubiri katika Hekalu. Hata hivyo, walipowashika na kuwakataza kuhubiri, jambo moja ambalo hawakukubali ni kwamba mitume hao walikuwa wakitenda muijiza wa kweli wa uponyaji.

Katika kina cha huduma hii ya uponyaji kuna kitu cha kawaida kabisa. Ni kile kipawa cha Roho Mtakatifu katika Kanisa la Agano Jipya. Tazama mfumo katika kizazi cha kwanza cha Kanisa: Ni kwa sababu tu ya Uwezo uliopewa Kanisa ambao unaona Matendo yaliyopewa Kanisa ambayo hayawezi kubishwa na ulimwengu.

## Mtindo Wa Kifo Kwa Ajili Ya Imani

Stefano, ambaye alikuwa amechaguliwa kama mmoja wa mashemasi wa kwanza, alivuka kutoka huduma ya utendaji hadi uchungaji na kuwa mhubiri mkuu. Huku akihubiri ujumbe wake mkuu mbele ya viongozi wa kidini wa Kiyahudi, ni dhahiri kwamba alikuwa akihubiri katika uwezo wa Roho Mtakatifu. Mahubiri si juhudi ya mtu binafsi wala kitendo cha werevu. Mahubiri ni kipawa cha kiroho, na ikiwa hayafanywi kupitia uwezo na upako wa Roho Mtakatifu, kwa hakika, sio mahubiri ambayo tunaona mtindo wake katika kitabu hiki.

Katika mahubiri haya, Stefano anatupatia ukaguzi wa vitabu thelathini na tisa kuanzia Agano la Kale. Anaonyesha ufahamu wa Maandiko. Anaanza na Ibrahimu; Isaka, Yakobo, na kugusia huduma ya Yusufu, Musa, Yoshua, Daudi na Sulemani. Pia, anagusia historia nzima ya Kiyahudi hadi katika uhamisho huko Babeli.

Kusudi la ujumbe wa Stefano sio uinjilisti, ingawa hapo baadaye ni ujumbe wenye mazao jinsi tutakavyoona baadaye. Kusudi la ujumbe wa Stefano ni kuwaeleza viongozi wa dini kwamba wao walikataa neema, upendo pamoja na wokovu wa Mungu. Kwamba wao walikuwa wamekataa kilicho chema ambacho Mungu alijaribu kuwatendea. Kilele cha kukataa kwao kilikuwa kumkataa Bwana Yesu Kristo, Masihi.

Huku Stefano akichambua historia ya Kiebrania kwa viongozi hawa wa kidini, kile alichokuwa akitilia mkazo ni kwamba kila mara walikataa Wokovu wa Mungu. Na matokeo ya ujumbe wa yalikuwa kama yalivyotarajiwa:

*'Basi waliposikia maneno haya, wakachomwa mioyo, wakamsagia meno. Lakini yeye akijaa Roho Mtakatifu, akakaza macho yake, akitazama mbinguni, akauona utukufu wa Mungu, na Yesu akisimama upande wa kuume wa Mungu. Akasema, Tazama! Naona mbingu zimefunguka, na Mwana wa Adamu amesimama mkono wa kuume wa Mungu. Wakapiga kelele kwa sauti kuu, wakaziba masikio yao, wakamrukia kwa nia moja, wakamtoa nje ya mji, wakampiga kwa mawe. Nao mashahidi wakaweza nguo zao miguuni pa kijana mmoja aliyeitwa Sauli.*

*Wakampiga kwa mawe Stefano, naye akiomba, akisema, Bwana Yesu, pokea roho yangu. Akapiga magoti, akalia kwa sauti kuu, Bwana, usiwahesabie dhambi hii. Akiisha kusema haya akalala. Na Sauli alikuwa akiona vema kwa kuuawa kwake.'*

Huku Stefano akifa kwa ajili ya ujumbe wake, anatuonyesha kwamba alikuwa amejawa na Roho Mtakatifu. Alikuwa na maono makuu ya Mungu na Kristo. Naye akafa kwa njia ambayo Bwana wake alikuwa amemtayarishia, akiwaombea msamaha wale waliokuwa wakitoa uhai wake.

Kwenye mahali pale alipopigiwa mawe Stefano, tunampata mmishionari mkuu, mpanzi mkuu wa Kanisa, mchungaji, mwalimu na mwandishi mkuu katika historia ya Kanisa la Yesu Kristo. Wakati tunapokutana na yeye, ana mavazi ya watu wale waliompiga Stefano mawe hadi kufa. Yeye ni Sauli wa Tarso, ambaye alifanyika mtume Paulo.

Tunapofikia kumfahamu huyu kijana Sauli wa Tarso, tunatambua jinsi ujumbe na mfano wa Stefano ulivyogusa maisha yake. Sauli alikuwa 'farisayo wa mafarisayo' naye alikuwa mfuasi sugu

wa dini aliyejitolea kuhifadhi itikadi za imani ya Kiyahudi. Alichukia kile alichodhania kuwa dini jipya ambalo lilitisha dini ya Kiyahudi.

Hata hivyo, kwa kuvutiwa na tabia ya kumuiga Kristo, Stefano ambaye alikuja kwa ajili ya imani yake, huku akiwa msomi mkuu wa Maandiko ya Kiyahudi, alivutiwa na kushawishiwa na ukaguzi mfupi na matumizi ya historia ya Kiyahudi kama yalivyoelezwa katika ujumbe wa Stefano.

Je! Wewe ungejitolea hili kufa kwa ajili ya Yesu Kristo jinsi Stefano alivyofanya? Je! Utakuwa na neema ya kutosha hata kuwasamehe watesi na maadui zako? Yamkini swali ngumu zaidi ni, 'Je! Wewe uko tayari, kwa neema ya kuishi kwa ajili ya Yesu Kristo?'

## Sura Ya Nne

## 'Jinsi Ya Kufanya Wanafunzi'

Hakika, tunafanya wanafunzi kwa njia gani? Kuna hadithi ya kuvutia sana katika kitabu cha Matendo ambayo inajibu swali hilo (Matendo 8:26-40). Kuna mtu mmoja kwa jina Filipo, ambaye kama mwenziwe Stefano, alikuwa mmoja wa wa lile kundi la kwanza la mashemasi. Alifanyika mfano mwingine wa mwaminifu mwenye mfumo wa karama ya kiroho cha utendaji ambaye alivuka hadi upande wa uchungaji wakati alipofanyika mwinjilisti. Anasafiri hadi Samaria na kuhudumu katika injili iliyokuwa na mengi sana.

Kwa wakati huu wenye mazao makuu katika mikutano ya uinjilisti, kupitia malaika, Bwana anamshauri Filipo: *'Ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza; nayo ni jangwa* (Matendo 8:26).' Ingawa wainjilisti wakati mwingi huenda mijini, Filipo alitii na kwenda nyikani.

Wakati Filipo alipowasili kule nyikani, aliona msafara wa magari ya kifalme yakifuatana huko nyikani. Roho alimwongoza hadi kwenye gari moja. Lugha ya Kiyunani katika kifungu hiki inaonyesha 'kwamba gari hili lilikuwa tofauti na zingine.' Hivi ndivyo tunafahamu kwamba kulikuwa na msafara wa magari. Wakati Filipo alipokaribia lile gari, alimpata mweka hazina wa nchi ya Kushi akisoma chuo cha nabii Isaya sura ya hamsini na tatu!

Ni wazi kuwa alikuwa amesafiri kutoka nchi ya Kushi hadi Yerusalemu kwa kuwa alikuwa na kiu cha roho. Alipowasili huko Yerusalemu, alikumbana na dini ile ile isiyo na upendo ambayo Yesu

mwenyewe alikumbana nayo. Hakuupata ukweli wa kiroho huko Yerusalemu, lakini alibahatika kupata nakala ya chuo cha Isaya. Alikuwa akisoma kwa sauti maneno haya: *'Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; Na Bwana ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote. . .* (Isaya 53:6,7,8).**'**

Filipo alimwuliza: 'Je! Yamekuelea hayo unayosoma?' Naye towashi huyo wa Kushi akajibu, *'Nitawezaje kuelewa, mtu asiponiogoza?* (30,31).**'** Naye Filipo akapanda kwenye gari lile na kusafiri pamoja, huku akimwelezea maana ya kifungu kile kutoka Isaya, kwamba kilikuwa kikinena na kutangaza Injili ya Yesu Kristo.

Ni dhahiri kwamba Filipo alifikisha ukingoni matoleo ya Injili kwa kukata kauli na kumwambia kwamba Imani katika Yesu inatangazwa kwa ubatizo wa maji. Tunasoma kwamba yule mtu kutoka Kushi alisema, *'Tazama, maji haya; ni nini kinachonizua nisibatizwe?' Filipo akasema, Ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana.'*

Hili ndilo jambo muhimu ya ubatizo katika maji: 'Amini kwa moyo wako wote.' Tunataja hili kama 'Ubatizo wa mwaminifu.' Kanisa limegawanyika jii ya namna ya kubatiza waumini. Hata hivyo, kilicho muhimu katika ubatizo sio njia ya ubatizo ila ni maana ya ubatizo huo. Agizo Kuu inahitaji kusomwa hivi, 'kufanya wanafunzi, kwenda, kuhubiri, kubatiza na kufundisha wanafunzi wale.'

Ubatizo ni kama sherehe ya harusi. Wakati mwanamume anapomchukuwa mwanamke kumuoa, naye anakubali kuolewa, huo ni wakati wa maana kwao wawili. Wakati wanapooana, huwakaribisha jamaa zao na marafiki zao katika sherehe ambayo huwa imetangazwa kwa umati wote. Wakati mtu kama huyo kutoka Kushi anapoamini, huko ni kujitolea kwa kibinafsi ambako hutangazwa kwenye umati wote anapobatizwa.

Wakati Yesu alipofanya ubatizo kuwa sehemu ya Agizo Kuu, aliufanya kuwa kitu kisichowezekana kwa kila mmoja wetu kumfuata na kufanya ahadi zetu kuwa za siri. Je! Mtu hukiri imani yake vipi? Je! Tunahitajika kuungana na Kanisa? Je! Sisi huitika kulingana na mwito wa mwinjilisti? Ni jambo la muhimu kutambua kwamba ubatizo hautupi wokovu, ni kukiri kuhusu imani yetu kulingana na amri ya Yesu.

Hadithi Kuhusu Petro

Kabla ya kutazama kuokoka kwa Sauli wa Tarso (Sura ya 9), ni lazima kwanza tutazame hadithi kuhusu Petro (Sura ya 10,11) ambayo inahitajika kukaguliwa pamoja na hadithi ya Filipo, kwa sababu hadithi hizi mbili zinatuonyesha ya kumfanya mtu kuwa mwanafunzi. Huku Petro akiwa amelala kwenye dari ya nyumba, anapokea maono ya shuka ambayo ilikuwa imefungwa pande nne. Katika shuka lile, walikuwemo wanyama wengi ambao Wayahudi walikuwa wamekatazwa kula. Na kwa mara tatu, sauti ilimjia Petro ikisema, '*Ondoka, Petro uchije ule* (10:13).' Kila mara, Petro anasema, '*Hasha, Bwana, kwa maama sijakula kamwe kitu kilicho kichafu au najisi.'*

Baadaye, kuna mtu mwenye kubisha mlango huko chini. Roho Mtakatifu anamfanya Petro kufahamu kwamba anahitajika kufuatana na watu waliokuwa wakibisha mlango huo, bila kuuliza maswali. Watu hawa ni watumishi wa akida wa kirumi jina lake Kornelio. Wao wanasema kwamba Bwana wao alikuwa na maono wakati alipokuwa akiomba na kwamba alijilishwa katika maono yale kuwatuma watumishi wake katika nyumba ya Simoni mfua ngozi na kumwuliza mtu aitwaye Petro ambaye angelikuja na kuieleza nyumba yake jinsi wangepokea wokovu.

Tilia maanani pingamizi zilizomo katika ubaguzi Petro aliokumbana nao. Huyu Kornelio hakuwa tu mtu wa mataifa. Pia, alikuwa adui wa Petro. Wayahudi walitambua watu wa mataifa kama mbwa koko kwa kuwa waliamini kwamba mtu ye yote asiye Myahudi ufahamu wake kuhusu Mungu ulikuwa kiasi cha mbwa koko. Kwa hakika, ilikuwa mwiko kwa Myahudi ye yote kumtembelea mtu wa mataifa asiye wa Kiyahudi. Hapa tunamwona Petro akiongozwa kuhubiri wokovu katika nyumba ya akida wa kirumi na wa kimataifa pia!

Wakati Petro alipowasili katika nyumba ya Kornelio, alipata tayari Kornelio amekusanya watu wa jamii na nyumba yake pamoja hili kumsikiliza akihubiri Injili. Petro alidhihirisha kwamba wakati huu, anafahamu maana ya maono yale. Wale wanyama waliokuwa najisi walikuwa watu hao– wa mataifa. Maneno ya kwanza ya Petro yalikuwa, *'…..lakini Mungu amenionya, nisimwite <u>mtu</u> awaye yote mchafu wala najisi* (28).'

Huku Petro akiendelea kuhubiri Injili, kuna tukio ambalo linatendeka ambalo linafanana na siku ya Pentekoste. Tunasoma kwamba, *'Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliosikia lile neno. (44).'* Katika sura inayofuatia, wakati Petro anapowaeleza mitume pamoja na waaminifu wengine jinsi Roho Mtakatifu alivyoshuka juu ya nyumba ya Kornelio,

anaongeza maneno haya, *'Na kama kwetu hapo mwanzoni (22:25).'* Ni jambo kuu kwamba Pentekoste hii ilitukia wakati Yesu alipokuwa akivuka mipaka ya ubaguzi na mgawanyiko katika Uyahudi na mataifa ya ulimwengu huku akijenga Kanisa Lake.

## Mnyororo Wenye Viunganisho Vitatu

Katika hadithi hizi za Filipo na Petro, tunapata kanuni ambayo inatuonyesha jinsi ya kufanya mwanafunzi. Mifano hii yenye uvuvio inatuonyesha kuwa kulikuwepo na 'mnyororo wenye viunganisho vitatu' kati ya Mungu na wale waliokuwa wamepotea. Kiunganisho cha kwanza kilikuwa Roho Mtakatifu. Kiunganisho cha pili ni Neno la Mungu na cha tatu ni mtumishi wa Mungu – yule anayewafanya wanafunzi.

Hili kumfanya mtu kuwa mwanafunzi, ni lazima Roho Mtakatifu afanye kazi ndani yake, hata kumfanya yule mfanya wanafunzi, kueleza Injili ya Yesu Kristo kwa mtu mmoja. Ni lazima pia Roho Mtakatifu awe akifanya kazi ndani ya aliyepotea, akileta njaa ya kiroho jinsi alivyofanya ndani mwa yule towashi kutoka Kushi na yule akida wa Kirumi.

Neno la Mungu, au Injili lazima iwepo tayari mahala pake, kama chombo ambacho Mungu ameahidi kutumia kufanya wanafunzi. Wakati mbegu ya Neno la Mungu linapookelewa katika moyo kwa imani, utungaji wa kiroho unatokea (1 Petro 1:22, 23).

Baadaye, mtumishi wa Bwana, au mfanya-wanafunzi, ni lazima aweo hapo. Anayetaka, aliyepo na mwaminifu, mfanya-wanafunzi – kama Filipo na Petro – ndicho kiunganisho cha tatu na chenye umuhimu sana kati ya Mungu na watu waliopotea. Ni jambo la kufurahisha kufikiri kwamba Mungu huwachagua watu kama wewe na mimi hili kuwa waakilishi wake katika kuishiriki Habari Njema na wale waliopotea.

Kuna ushahidi kuonyesha kwamba Roho Mtakatifu anafanya kazi katika maisha ya waliopotea, ambao bado hawajawahi kusikia wala kuipokea Injili? Katika mifano hii miwili, Luka anatupatia ishara za matendo ya kiroho ambayo ni dhahiri kabisa. Yamkini inawezekana kwamba matendo haya ya kiroho si wazi katika kushirikiana na watu waliopotea, ingawa tunaweza kuona wakati tutakapokuwa tukiomba na kutafuta ishara hizo.

Swali nzuri ambalo litatuongoza vyema kwenye mazungumzo hadi tutakapoweza kushiriki Injili ni: 'Je! Wewe unashughulikia mambo ya kiroho?' Jambo ambalo si jema ambalo linaweza kutokea katika kujibu swali hilo ni kuwa, 'La, Hasha!' Ikiwa una imani na ujasiri wa kuuliza swali hili, utatambua kuwa watu wengi wana shauku kuu katika mambo ya kiroho. Watu waliopotea wanahitaji mtumishi wa Mungu ambaye yuko tayari 'kupanda kwenye gari' pamoja nao, na kuwasaidia kufahamu jinsi Neno la Mungu linavyosema ambalo linahusika kwao kwa njia ya uzima wa milele.

Unapoona ishara za Roho Mtakatifu zikitenda kazi katika maisha ya mtu aliyepotea, naye Roho akikuongoza kushiriki katika Injili nao, je! Unataka kuwa kiunganiso cha tatu katika mnyororo ulio kati ya Mungu na mtu aliyepotea? Mimi niliazimia na kujitolea kwa Mungu, huku nikifikiria kwamba singekutana na watu wengi kama yule akida wa Kirumi na towashi kutoka Kushi. Lakini nilikuwa nimekosea. Tangu wakati nilipofanya uamuzi huo kwa Mungu miaka mingi iliyopita, nimekutana na watu wengi kama hao na nimeona wengi wakija katika imani kwa Kristo na kuwa na kushuhudia kuzaliwa mara ya pili.

Nilipokuwa mchanga katika imani, nilikuwa mtu mwenye kuona haya, bila ujasiri wala kujiamini mwenyewe wakati nilipoanza kuitika mwito na mwongozo wa Roho Mtakatifu hili kuishiriki katika Injili na watu binafsi. Nilipoelewa dhana ambayo inaeleza kuwa ni mnyororo wenye viunganisho vitatu, nilitiwa moyo wa kutambua kisha kuthibitisha mara nyingine kwamba viunganisho viwili vya kwanza katika mnyororo huu vina nguvu sana, na kwamba wokovu wa mtu aliyepotea hautengemei akili wala elimu, uweza wetu wa usanifu na ushawishi au 'uuzaji wetu.'

Sisi ndio kiunganisho dhaifu katika mnyororo huu, lakini kwa sababu ambazo sifahamu, ingawa Mungu anaweza na wakati mwingi, hufanya muijiza huu bila sisi, amechagua kutumia kiunganisho hiki dhaifu cha kibinadamu hili kuleta watu waliopotea katika imani na wokovu. Kristo aliyefufuka na anayeishi ni mzabibu unaotafuta matawi ambayo kwayo, anaweza kuzaa '*matunda yanayodumu* (Yohana 15:16).'

Je! Wewe umewahi kushiriki katika habari njema na watu wengine? Je! Wewe ni mtiifu kwa ile Agizo Kuu iliyotolewa na Kristo? Ikiwa sivyo, ninakupa changa moto kumwuliza Mungu akuonyesha jinsi tayari anavyotenda kazi katika maisha ya wale wanaoishi karibu nawe. Kisha mwulize akupatie ujasiri wa Petro na Filipo katika kushiriki katika ujumbe wa neema na rehema Zake pamoja na.

Unaposhiriki katika Injili, utakuwa na ufahamu wa furaha ya kumtii na kutumiwa na Mungu. Wakati tunapotangaza habari njema ya Kristo kwa waliopotea, huwa tunatofautisha uzima wa milele katika maisha yao. Maombi yangu ni kwamba, tunaposoma kitabu hiki cha Matendo, utapakwa mafuta ya uwezo wa Roho Mtakatifu hili kushiriki kwa ujasiri katika Injili kama Petro na Filipo pamoja na Paulo na wengine tutakaowasoma katika kitabu hiki.

## Sura Ya Tano
## 'Pentekoste Ya Kibinafsi Ya Paulo'

*'Lakini Sauli, akizidi kutisha na kuwaza kuwaua wanafunzi wa Bwana, akamwendea Kuhani Mkuu, akataka ampe barua za kuenda Dameski zilizoandikwa kwa masinagogi, ili akiona watu wa Njia hii, waume kwa wake, awafunge na kuwaleta Yerusalemu.*

*'Hata alipokuwa akisafiri, ikawa anakaribia Dameski; ghafula ikamwangaza kote kote nuru kutoka mbinguni. Akaanguka chini, akasikia sauti ikimwambia, Sauli, Sauli, mbona waniudhi?*
*'Akasema, U nani wewe, Bwana? Naye akasema, Mimi ndimi Yesu unayeniudhi wewe. Lakini simama, uingie mjini, nawe, utaambiwa yakupasayo kutenda (Matendo 9:1-6).'*

Maneno haya ambayo yafahamika sana na watu wengine, yanaeleza kuokoka kwa Sauli wa Tarso na ni ushuhuda ambao unajulikana kama 'Ushuhuda wa njia ya Dameski.' Hauwezi kufafanua mtu huyu isipokuwa kwa neno 'ushuhuda.' Jinsi tayari tumeona, wakati tunapokutana naye, yeye ni mchukiaji mkuu wa wakristo, lakini huu ushuhuda katika njia ya Dameski ni mojawapo ya baadhi ya ushuhuda ambao ulimfanya kuwa mtume (mmishionari mkuu) katika historia ya Kanisa la Yesu Kristo.

Zipo sehemu kadha katika kitabu cha Matendo ambapo Paulo atatueleza kuhusu ushuhuda wa kwanza. Mbele yao, makutano yenye upinzani, mbele ya wakuu na mfalme na malkia, katika mahakama ya dini, na katika nyaraka zake ambazo zimevuviwa, Paulo anaendelea kutuambia, 'nilikuwa na ushuhuda.'

Kwa hakika, Paulo anatuambia kuhusu ushuhuda mara tatu ambao ulimfanya kuwa mtume mwenye mazao mengi katika historia ya Kanisa. Ushuhuda wake wa kwanza ulikuwa ule wa kuokoka akiwa njiani kuelekea Dameski. Alikuwa na ushuhuda mwingine katika jangwa huko Arabuni, ambao anaeleza kwa usanifu na uwazi kabisa katika waraka wake kwa Wagalatia (1:11-22:10). Pia, alikuwa na ushuhuda mwingine wa mbinguni ambao uligusia sana maisha yake. Naye anashiriki katika ushuhuda huo na Wakorintho pamoja nasi (2 Wakorintho 12:1-4). Yawezekana kwamba wakati alipopigwa kwa mawe huko mjini Listra (Matendo 14:19,20).

Ushuhuda huu wa mbinguni ulimshawishi Paulo kwamba sio lazima tungojee hadi wakati tutakapokufa hili tuweze kuishi mbinguni. Somo kuu katika waraka huu kwa Waefeso ni, 'katika maeneo ya mbinguni' ambako alimaanisha kwamba maisha yetu hapa ulimwenguni (Waefeso 1:3). Kwa hakika, hatuwezi kufananua mtu huyu asiye wa kawaida kwa njia nyingine isipokuwa kuambatana na shuhuda hizi tatu.

Kuna mambo machache ambayo tunahitajika kutambua kuhusu ushuhuda wa kwanza wa mchukiaji mkuu wa Kristo. Kwanza, Sauli anasikia sauti ikimwita kwa jina lake na kumwuliza, *'mbona wewe waniudhi?'* Hapa kwa mara nyingine, tunamwona Kristo aliyefufuka akiwa hatengwi mbali na Kanisa Lake. Paulo alikuwa akitesa Kanisa, lakini swali la Kristo aliyefufuka ni, 'mbona wanitesa au kuniudhi mimi?' Ujumbe dhahiri ni kuwa: 'Wewe waniudhi mimi wakati unapoliudhi Kanisa langu.'

Sauli naye anajibu kwa swali, 'Wewe ndiwe nani, Bwana?' Yeye hakumfahamu aliyekuwa akizungumza naye, ila alifahamu kwamba aliyekuwa akizungumza naye ni Bwana wake.

Katika wokovu wa Sauli, kuna mfano na fumbo ambalo linatusaidia kufahamu dhana kuhusu 'unyenyekevu.' Katika hadithi hii, tunajifuza kwamba unyenyekevu kwa hakika ni 'kufugwa.' Farasi ambaye hajavunjwa na kutiishwa,wala kutiwa lijamu kwenye mdomo wake, au hitamu juu ya kichwa chake na kutandikwa mgongoni, anahitaji afugwe na kutiishwa. Wakati farasi huyo anapofugwa, na kufikia mahali ambapo hataivuta ile lijamu, ila ataelekea kule lijamu na hitamu zinapoelekezwa. Hii haimaanishi kuwa mnyama yule ni mnyonge. Mnyama aliyefugwa ni mnyama mnyenyekevu.

Wakati Kristo aliyefufuka anapomwelezea Sauli, 'ni vigumu kuipiga miiba,' anamaanisha, 'mbona wewe waivuta lijamu? Itakupasua midomo yako. Ina maumivu kwako.' Fumbo hili linaonyesha kwamba, kabla ya ushuhuda huo wa Dameski, Roho Mtakatifu tayari alikuwa

akishughulikia Sauli wa Tarso, akimzungumzia kupitia ushuhuda wa Stefano na wale waumini walioteswa. Sauli anatuonyesha kwamba anakubali ule uongozi wa lijamu na hitamu au kufanyika mnyenyekevu, wakati anapouliza, '*Bwana, ni kitu kipi ambacho unataka nitende?* (6)'

Katika nyaraka za Paulo na zaidi ya mtu mwingine, atatuambia kwamba Mungu ametutendea katika kutupa wokovu kupitia Kristo. Lakini wakati anapokutana na Yesu, swali lake sio, 'Wewe utanitendea nini?' Swali lake kwa hakika ni, 'Bwana, ni kipi ambacho unataka mimi nitende kwa ajili yako?'

Kama matokeo ya wokovu wake, mtazamo wa Paulo wa maisha ulibadilika kabisa. Pamoja na mambo mengine, yeye alibadilisha jina lake. Jina lake la Kiebrania Sauli linamaanisha 'mwenye nguvu' au 'mkuu.' Wakati alipookolewa, aliamua kutumia jina la Kirumi, Paulo.

Yawezekana kwamba humu yake ilikuwa kwa sababu alikuwa na mwito wa kuwafikia watu wa kimataifa kote katika milki ya Kirumi. Kwa kuwa alikuwa mzaliwa wa Kirumi, na alitaka kila kitu kwa kila mtu, ilikuwa jambo la busara kubadilisha jina lake la Kirumi. Hata hivyo, hatuwezi kupuuzia kwamba Sauli ilimaanisha mkuu au mwenye nguvu, na Paulo ilimaanisha, 'aliye duni' au 'asiye kitu!' Wakati Sauli alipobadilishwa na kuwa Paulo, ni dhahiri kwamba alipokea ushuhuda '*masikini wa roho (Mathayo 5:3).'*

Baadaye, aliandika kwa Wafilipi kuwa: *'….Lakini mambo yale yaliyokuwa faida kwangu, naliyahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya Kristo. Naam, zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu; ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo….* (Wafilipi 3:1-11).'

Jambo la muhimu pale ushuhuda unapohusika sio yaliyomo katika ushuhuda huo. Bali ni: Matokeo gani yaliyo katika ushuhuda huo? Ushuhuda huo sio mwisho ila ni namna tu ya kufikia mwisho huo. Ushuhuda kwa hakika, ni mlango ambao tunapitia hili kuwa watumishi bora wa Kristo. Katika kitabu cha Matendo, Paulo anatuambia matukio yaliyokuwepo katika ushuhuda wake njiani kuelekea Dameski mara kadhaa. Kile anachoandika kwa Wafilipi kinatilia mkazo matokeo ya ushuhuda wake wa njia ya Dameski.

Baadhi ya waaminifu ni wale wanaotajwa kama wa 'kutafuta faida.' Faida ni mambo yale ambayo hutumiwa. Waaminifu wanaweza kumtumia Mungu jinsi tunavyotumia maji, mishumaa, umeme, baisikeli au magari ya abiria mjini. Bila hata kutambua, tunaweza kufanyika wafuasi wa Kristo kwa sababu tunaamini kwamba atasuluhisha matatizo yetu yote. Kwa hakika, tunapomfuata Kristo, Yeye hutatua matatizo yetu yaliyo makuu. Lakini hebu ni kuulize swali: 'Unapomfuata Kristo, je unamwuliza kile ambacho atakutendea au kama Paulo unamwuliza Bwana na Mwokozi wako kile ambacho anahitaji wewe kutenda?'

Baada ya hadithi hiyo ya wokovu wa Paulo, tunasoma juu ya 'kufuatilia' wokovu wake. Mungu anamwendea mkongwe aitwaye Anania na kusema, '*Mimi nataka wewe kwenda hili umbatize mtu aitwaye Sauli wa Tarso.'* Jina hili Sauli wa Tarso lilimtia hofu moyoni mwake. Naye akajibu, *'Bwana, nimesikia habari za mtu huyu kwa watu wengi, mabaya mengi aliyowatendea watakatifu wako Yerusalemu; hata hapa ana amri itokayo kwa wakuu wa makuhani awafunge wote wakuitiao Jina lako* (Matendo 9:13, 14).' *Naye Mungu akamwambia, Nenda tu; kwa maana huyu ni chombo changu kiteule kwangu, alichukue Jina langu mbele ya Mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli (15).'*

Huku akizungumza kwa njia ya mafumbo, Mungu anafungua chuo na kumwonyesha Anania mpango Wake kwa maisha ya Sauli wa Tarso. Hebu tambua kwamba, Mungu hatendi hivyo kwa Sauli. Yeye kwa urahisi, amwambia Sauli*: 'Simama, uingie mjini, nawe utaambiwa yakupasayo kutenda (6).*' Matumizi ya kibinafsi katika kuabudu kwetu kutoka hapa ni kwamba, Mungu anaweza kutuonyesha mapenzi Yake yote kwa maisha yetu kama angelipenda. Lakini hatendi hivyo. Yeye hudhihirisha mapenzi Yake kwetu kama alivyodhihirisha kwa Sauli – siku moja baada ya nyingine na mwongozo mmoja kwa wakati mmoja.

Maneno yenye kuvutia katika kitabu cha Matendo ni yale yaliyonenwa na Anania wakati alipokwea katika chumba ambacho Sauli wa Tarso alikuwa akimgojea. Punde tu wakati Anania alipofahamu kwamba huyu adui mkuu wa Kanisa alikuwa amebadilishwa, asema, 'Ndugu Sauli.' Kile tunachoshuhudia hapa katika Kanisa la Yesu Kristo ni: Neema ya Mungu ya kubadilisha maisha!

## Ushuhuda Wa Jangwani Wa Paulo

Tunakumbana na utaratibu wa changa moto wakati tunaposoma hadithi ya ushuhuda wa kubadilishwa kwa Sauli. Huwa tunafikiria kwamba baada ya kubadilishwa huko kwa Paulo, alianza kuhubiri kwa ujasiri kwa jina la Yesu huko Dameski na Yerusalemu. Hata hivyo, ni lazima tuweke

kimya kirefu kati ya kubadilishwa kwake na huduma yake. Ni lazima tujumuishe kile anacho waambia Wagalatia kuhusu kwenda Arabuni baada ya kuokoka kwake (Wagalatia 1:11-21).

Wasomi hawakubaliani juu ya muda ambao Paulo alikuwa katika ushuhuda huu wa jangwani, ilhali wengi wanakubaliana kwamba alikiri kuwa alikuwa huku kwa kipindi cha miaka mitatu. Paulo anakiri kwamba Kristo aliyefufuka alikuwa pamoja naye kwa miaka mitatu akimfunza yale yote aliyoandika katika nyaraka zake, ambazo huchukua nusu ya Agano Jipya. Baadaye, alikwenda Dameski, na hatimaye mji alikozaliwa wa Tarso.

Paulo atuambia kwamba baada ya miaka kumi na minne tangu kubadilishwa kwake, alikwea hadi Yerusalemu na kukutana na mitume wale wengine wote kwa mara ya kwanza (Wagalatia 2:1-20). Ni dhahiri kwamba Paulo aliwashawishi kwamba alikuwa na Yesu kwa muda wa miaka mitatu jinsi wao walivyokuwa naye. Ni lazima kwamba yeye alikuwa amewaambia vitu ambavyo ni wale tu waliokuwa karibu naye wangefahamu. Ndipo wakaamua Paulo ahubiri Injili kwa ulimwengu wa mataifa, na wale mitume wengine wawahubirie Wayahudi.

Kama ingekuwa mimi, nisingefanya hivyo. Ningemtuma Paulo, rabii na msomi aliyeokoka kwao Wayahudi, kisha wale ambao hawakuwa na elimu ya juu, kama Petro, Yakobo na Yohana kwa watu wa mataifa wasio staarabika. Lakini Mungu haitendi kazi hivyo kama wanadamu. Yaonekana kuwa Yeye hupendelea kutumia watu wa kawaida kutenda mambo yasiyo ya kawaida. Yeye alimtuma yule Rabii aliyeokoka na msomi kwa wapumbavu wa kimataifa na mitume wasio na elimu kwa wasomi na Warabi.

Yamkini nusu ya kitabu cha Matendo inadhihirisha Petro kuwa kiraja mtume, ilhali nusu ile nyingine inatambulisha maisha na kazi ya mtume Paulo. Unaposoma hadithi ya kuokoka kwa Paulo katika kitabu hiki cha historia, hakikisha umeacha kwa muda mfupi, hili usome madai yake ya ushuhuda wa jangwani kitabu cha Wagalatia sura ya kwanza na ya pili. Wakati anapotoa madai hayo kwa Wagalatia, anatangaza kuwa, ‘mbele za Mungu, Mimi sisemi uongo.’

Ni lazima ufanye uamuzi kuhusu Paulo.  Aidha kwamba Paulo ni msema uongo au ni mtume. Kwa hakika, yeye anadai kwamba alitenda kazi zaidi ya mitume wengine wote. Yeye ndiye mwandishi wa zaidi ya nusu ya vitabu katika Agano Jipya ambavyo tutavichambua wakati tutakapomalizia uchunguzi wa kitabu hiki cha Matendo. Hifadhi maoni yako kuhusu Paulo hadi wakati

utakapokuwa umesoma na kwa uangalifu, kutilia maanani mambo makuu yaliyomo katika nyaraka hizi zilizovuviwa.

Nilianza kusoma Biblia yangu mnamo mwaka wa 1949 kwa kusoma nusu ya pili ya kitabu cha Matendo kwa matayarisho ya ukaguzi wa nyaraka zake zote zilizovuviwa. Nimeshawishika kabisa kwamba ni Kristo aliyefufuka tu ambaye angeweza kumfunulia mtu huyu wa kushangaza asiye wa kawaida wa Mungu ukweli mkuu ninaozidi kupata kwa miaka mingi katika nyaraka zake.

## Kutana Na Barnaba

Luka anatilia mkazo ju ya kazi ya Paulo na Petro wakati anapoandika historia ya kizazi cha kwanza cha Kanisa. Hata hivyo, kwa ziada juu ya hawa viongozi wawili, kuna watu wengine ambao anafikiri kuwa unahitaji kuwafahamu hili kuelewa vyema chanzo cha Kanisa la Kristo. Mmoja wao ni Barnaba, ambaye jina lake linamaanisha, '*mwana wa faraja (4:36).'*

Kufuatia mfano wa Yesu, mitume walibadilisha jina lake kutoka Yusufu hadi Barnaba, ambalo linaeleza mfumo wa karama yake ya kiroho pamoja na huduma yake. Kila mara tunamwona akiishi katika kutimiza yale yote yaliyotarajiwa kutoka kwake, kulingana na jina lake jipya alilopewa, huku kwa uaminifu akiwaunga mkono na kuwafariji wao kutenda lile Bwana wao aliyowaita kutenda. Barnaba alikuwa msaidizi wa Paulo katika uanzishaji wa huduma ya kimiujiza ya umishionari.

Tunasoma kwamba alikuwa akitenda kazi katika Kanisa la Antiokia, akiwafanya waumini wapya kuwa wanafunzi. Kanisa lilikuwa na ushuhuda mkuu wa kukua kwake katika hesabu ya waumini kwa kuwa Roho Mtakatifu alikuwa akitenda pamoja naye kwa uwezo mkuu. Walikuwepo waumini wengi wapya kiasi kwamba Barnaba alitambua kwamba Kanisa hilo lilihitaji huduma ya mafunzo ya kipekee ya Rabii aliyeokoka, Sauli wa Tarso. Hivyo basi, alikwenda hadi huko Tarso na kumtafuta hadi kumpata Paulo, kisha akamleta hadi Antiokia na kumtawaza katika huduma ya ufundishaji. Tunasoma kwamba Barnabas ndiye aliyemtetea aliyekuwa adui wa Kanisa pamoja na waumini wengine, ambao walitilia shaka sababu ya kumleta Paulo huko Antiokia (Matendo 9:26).

*Inatubidi kukumbuka kwamba mtume Petro hangekuwepo kama sio kwa Andrea. Ni Andrea aliyemleta nduguye Simoni na kumtambulisha kwa Yesu. Andrea anaonyeshwa kwa mara nyingine akitenda kazi moja kwa moja kwa kuwaleta watu kwa Yesu kwani ni yeye anayegundua yule kijana mdogo aliyetoa chakula chake cha mikate midogo mitano na samaki wawili wadogo na kuwalisha*

*makutano makubwa ya watu wenye njaa. Kwa njia hiyo, tunaweza kusema kwamba Paulo hangehudumu kama sio kwa 'mwana wa faraja' Barnaba.*

Paulo na Barnaba wanatengwa na kutumwa na Kanisa la Antiokia hili kuanza safari nyingi zao zenye mazao mengi wakiwa pamoja (Matendo 13:1-3). Hata hivyo, walipokuwa katika matayarisho ya safari ya pili ya umishionari, kulitokea mashindano kati yao na wakatengana katika huduma yao kama washirika ambao walikuwa wamefungwa nira pamoja na Kristo kwa yule mwingine. Barnaba anamtaka mpwaye Yohana Marko, kusafiri nao katika safari hiyo ya pili. Huyu Yohana Marko alikuwa nao katika safari ya kwanza, lakini baadaye alitoroka wakati dhiki alipoanza. Naye Paulo hakutaka kumchukuwa kwenda naye.

Ubishi huu kati ya Paulo na Barnaba ni mkuu sana kuhusu jambo hili, kiasi kwamba wanatengana. Paulo anamchukua Sila na kusafiri naye upande moja; hali Barnaba anamchukua Yohana Marko na kusafiri naye upande ule mwingine. Kote katika historia ya Kanisa hii imekuwa shida kuu kwa wamishionari. Yule muovu anafahamu kwamba hatuwezi kuvutia ulimwengu ikiwa hatuko pamoja. Hii ndio sababu Yesu alitilia mkazo kuhusu uhusiano wetu pamoja na ndugu zetu (Mathayo 5:23,24; 18:15-17).

Hata hivyo, ni muhimu kusoma baadhi ya maneno ya mwisho yaliyoandikwa na mtume Paulo akiwa gerezani lililoambawa sana la *Mamertine* huko Roma. Nyaraka hizo zilielekezwa kwa Timotheo: '*Mlete Yohana Marko pamoja nawe. Yeye ni mhuduma mwenye faida.'* Ni hadithi gani iliopo katika kijana huyu hata 'kuwa mhuduma mwenye faida?' Wasomi huamini kwamba jibu kwa swali hilo ni kuwa, Barnaba aliendelea kumhudumia Yohana Marko baada ya Paulo kukata tamaa. Yohana Marko afanyika kuwa mtu aliyeandika Injili ya pili kwa sababu Barnaba alikuwa 'mwana wa faraja.'

Kumekuwa, kuko na kutazidi kuwa watu wengi Kanisani ambao wanahitaji mtu wa kuwapa faraja katika hali ya uhusiano wao na mtu mwingine. Je! Wewe u tayari kuwepo pale kwa ajili ya mtu kama yule? Ikiwa u mwaminifu mchanga, basi unahitaji Barnaba. Ikiwa u mwaminifu aliyekomaa, unahitaji kumpa faraja na kumfunza Yohana Marko. Kila mara unapokuwa na fursa, kama Roho Mtakatifu akikuongoza, iga mfano wa Barnaba na kuwapa faraja wale wanao kuzingira – hasa waumini wapya – hili wawe kila kitu ambacho Bwana na Mwokozi wao anataka kuwa.

## Sura Ya Sita

## 'Mifumo Ya Pentekoste Ya Kupanda Kanisa'

Kulingana na Luka, kuna nyakati muhimu katika kuenezwa kwa Injili. Tunasoma kuhusu wakati mmoja katika sura ya kumi na sita. Huku Paulo akifanya safiri ya pili ya umishionari, anatamani kuingia huko Asia na kuhubiri Injili. Hata hivyo, tunasoma kwamba pamoja na wenziwe, walikatazwa na Roho Mtakatifu kuigia Asia. Nyakati za usiku, Paulo alipokea maono ya mtu kutoka Makedonia ambaye alikuwa akimsihi: '*Vuka uje Makedonia utusaidie.'*

Baada ya Paulo kupokea maono *hayo, tunafahamu kwamba Luka ameungana nao tunaposoma: 'Mara tukataka kutoka kwenda Makedonia, kwa kuwa tuliona hakika ya kwamba Mungu ametuita tuwahubiri Habari Njema.* (Matendo 16:7-10).' Ingawa Paulo pamoja na wenziwe wangesafiri hadi huko Asia hivi karibuni, ni muhumi kwamba wapate kufika Makedonia kabla ya kufika Asia.

Kwa wakati huu, Paulo anakuwa na huduma ya kwanza kwa Wagalatia. Unapotambua kwamba Paulo alikuwa akiwaandika Wagalatia kuhusu hali yake ya afya wakati huu, tunaweza kukubaliana kwamba Roho Mtakatifu alitumia hali ya afya ya Paulo kumkataza kusafiri huko Asia (Wagalatia 4:13-15). Hili linawezekana kwa sababu yule tabibu wake mpendwa Luka alikuwa ameungana naye wakati huo.

Mji wa kwanza waliotembelea baada ya kuingia huko Makedonia ulikuwa ni Filipi. Unaweza kufikiria kwamba kwa sababu ni mwanaume katika maono ya Paulo ambaye alimsihi, *'Vuka, uje Makedonia utusaidie,'* angewapata wanaume wengi wakiwa na hamu ya Injili. Badala yake, alipata kundi dogo la wanawake kwenye ufuo wa mto ambao walikuwa na mkutano wa maombi. Paulo kwa hakika, alianzia kwa kile ambacho kilikuwa dhahiri kwamba ni Mungu aliyekuwa amemtayarishia kuhubiri Injili kwa hawa wanawake wa Kiyahudi.

Mmoja wao alikuwa ni Lidia*, 'mwenye kuuza rangi ya zambarau (14).'* Hii inamaanisha kwamba alikuwa ni mshonaji wa mavazi ya kifalme. Tunasoma kwamba wakati Paulo alipofungua Neno la Mungu, naye Bwana *'akaifungua roho yake (14).'* Kisha akaifungua nyumba yake kwa Paulo pamoja na kundi la umishionari. Nyumba ya Lidia ilifanyika kuwa Kanisa la kwanza Uropa. Kulikuwa

na bado kuna majengo ya Makanisa yenye kuvutia sana huko Uropa, lakini huko mbinguni, huyu mshonaji anaweza kudai kwamba nyumba yake ilikuwa Kanisa la kwanza Uropa.

Ni katika mji huu wa Filipi ambako Paulo na Sila walishkakiwa na kufungwa gerezani hata kupigwa (22-24). Hata baada ya adhabu hii, tunasoma kwamba usiku wa manane Paulo na Sila waliomba na kumsifu Bwana kiasi kuwa wafungwa wote gerezani walipata kuwasikia wakiimba. Ghafula kulitokea tetemeko kuu! Minyororo ya wafunguwa ikaanguka chini, huku milango ikifunguka. Hili lilikuwa ni tetemeko la kushangaza sana!

Wakati mkuu wa gereza alipoamka kutoka usingizini na kushuhudia milango ya gereza ikiwa wazi, alichukua upanga wake akitaka kujiua, lakini Paulo akamwambia, '*Usijidhuru, kwa maana sisi sote tupo hapa!'* Naye akawauliza, *'Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?'* Naye Paulo akamjibu: '*Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe utaokoka - pamoja na nyumba yako.'*

Maneno yanayonifuatia tunayosoma ni: *Wakamwambia Neno la Bwana yeye pampja na watu wote waliomo nyumbani mwake. Akawakaribisha saa ile ile ya usiku, akawaosha mapigo yao, kisha akabatizwa, yeye watu wake wote wakati uo huo. Akawaleta juu nyumbani kwake, akawaandalia chakula, akafurahi sana, yeye na nyumba yake yote, maana amekwisha kumwamini Mungu* (28-34).'

Njia ya wokovu haijawahi kutajwa kwa uwazi mkuu kuliko vile ilivyo katika maneno haya: *'Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe utaokoka.'* Mimi niliokolewa na kufanyika mwanafunzi wa Yesu Kristo mnamo mwaka wa 1949 wakati niliposikia maneno hayo kwa mara ya kwanza. Naamini kwamba wakati huu Paulo alikutana na yule mtu aliyekuwa katika maono yaliyomwongoza hadi Makedonia.

Baada ya kuokolewa kwa yule mkuu wa gereza, wale wakuu walituma ujumbe kwamba ilimbidi Paulo kuachiliwa huru kisha ahame mji huo mara moja (35,36). Hata hivyo, Paulo alikataa kuahama mji huo kwa njia hiyo wala kwa wakati huo. Kwa kuwa alikuwa amepigwa kama raia wa Kirumi, na bila kufikishwa mahakamani, aliwataka wakuu hao waje na kumsindikiza binafsi pamoja na Sila hadi nje ya mji huo. Alihama mji huo kwa wakati wake na kwa njia yake mwenyewe.

Paulo hakumwona Kristo akibadilisha mji wa Filipi juu chini. Kanisa alilolipenda sana Paulo lilikuwa limeziduliwa katika mji wa Filipi. Kanisa hili lilikuwa ndio msingi mkuu na lenye usaidizi sana lililomwezesha kusafiri kote Makanisani yaliyokuwa katika miji mingine kama, Korintho, Efeso na Thesalonike. Anatumia mfumo wa uwakili mwaminifu wa kanisa la Filipi kama mfano kwa Makanisa *mengine (2 Wakorintho 8:9).* Paulo alikuwa akitenda kazi yake kama mtengezaji wa hema badala ya kupokea matoleo kutoka kwa waumini wale ambao hawakuwa wamekomaa katika haja zao, ambao walikuwa walitilia shaka dai lake kuwa ni mtume, hivyo basi hawakustahili kufanyika washirika pamoja naye katika huduma yake.

Unaposoma hadithi ya Paulo katika mji wa Filipi, usije ukasahau maneno haya: 'Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka – pamoja na nyumba yako.' Tambua kwamba maneno haya hutupa changa moto kumwamini Bwana Yesu Kristo. Yesu humaanisha kwamba tumwamini kama Mwokozi wetu. Kristo humaanisha tuamini Mwokozi wetu ni Masihi. 'Bwana' linamaanisha kwamba tumemfanya Masihi Mwokozi, Bwana na Mkuu wetu.

Je! Wewe unaamini kwamba Yesu ndiye Mwokozi wako? Ikiwa haujafanya hivyo, kwanza, 'Mwamini Bwana Yesu Kristo nawe utaokoka pamoja na nyumba yako.'

## Sura Ya Saba
## 'Mahubiri Ya Paulo'

Paulo alipowasili katika mji wa Athene, roho yake ilichukizwa sana ndani yake kwa kuona jinsi mji ule ulivyojaa sanamu (Matendo 17:16). Mwana historia mmoja alidai kwamba ilikuwa rahisi kupata sanamu huko mjini kuliko mtu. Kuabudu huko kwa sanamu kulimfedhehesha Paulo kwa kuwa alifahamu kwamba sanamu hizo hazikuwa Mungu, na kwamba watu hao hawangeweza kumjia Mungu wa kweli kupitia sanamu hao.

Paulo amejawa na dhiki kuu ambayo inawasilisha mpangilio mwafaka wa uinjilisti katika miji ambayo alieneza Injili. Wakati wote alikwenda kwenye Sinagogi kwanza na kutangaza kwa Wayahudi kwamba: 'Yesu ni Kristo.' Alikuwa Rabi mwenye hati za kudhibitisha hayo. Hivyo basi, angekwenda hadi kwenye sinagogi na kupokea ruhusa kisha kuhubiri na kufundisha Injili kwa Wayahudi. Huu ulikuwa mpangilio wa Paulo – '*kwa Wayahudi kwanza, kisha Wayunani (Warumi 1:16).'* Ingawa Paulo alikuwa ameitwa hili kuhudumu katika ulimwengu wa Mataifa, alikuwa na mzigo mkuu kwa

watu wa Kiyahudi, hivyo basi alihubiri kwanza kwa Myahudi. Tunaelewa sababu yake kwenda kwa Myahudi kwanza tunaposoma maelezo ya mzigo wake kwa Wayahudi katika waraka wake kwa Warumi (9:1-5).

Sehemu ya pili ya mpangilio wake ilikuwa kwenda sokoni na kushiriki katika Injili pale watu wengi walipokusanyika. Tunasoma kwamba, *'Waathene na wageni waliokaa huko walikuwa hawana nafasi kwa neno lo lote ila kutoa habari na kusikiliza habari za jambo jipya* (Matendo 17:21).' Wayunani walikuwa watu wenye elimu na falsafa. Wao walipenda ubishi na kuwa na hoja zenye uzito, dhana za kiakili na hasa alifurahia kusikiza cho chote kilichokuwa kipya.' Kwa hivyo, Paulo alikwenda sokoni kila siku na kushiriki katika Injili na kila mtu ambaye alitaka kumsikiliza.

Sehemu ya tatu ya mpangilio wake ilikuwa katika kuieneza Injili kwa wale waliokuwa wenye ushawishi mkuu katika jamii. Kwa kuwa Paulo alikuwa mmoja wa watu waliokuwa wenye elimu ya hali ya juu katika kizazi chake, alikuwa ni mwenye mazao mengi kwa kuwafikia viongozi. Alipokuwa akiutamiza mpangilio wake huko Athene, alikaribishwa katika eneo nzuri juu ya kilima cha Mars kilichojulikana kama Areopago. Areopago palikuwa mahali watu maarufu na wenye elimu walipokutanika hili kujadiliana juu ya hoja kuu. Mahali pale pia palitumiwa kama mahakama na palikuwa ni mahali ambapo ungeouna mji wote wa Athene kutoka pale. Wakati Paulo alipokaribishwa hili kunena katika Areopago juu ya mlima wa Mars, aliuhubiri ujumbe wenye usanifu mwingi sana. Alianza kwa kusema: *'Enyi watu wa Athene, katika mambo yote naona ya kuwa ninyi ni watu wa kutafakari sana mambo ya dini. Kwa sababu nilipokuwa nikipita huko na huko na kuyaona mambo ya ibada yenu, naliona madhabahu iliyoandikwa maneno haya, KWA MUNGU ASIYEJULIKANA. Basi mimi nawahubiri habari zake yeye ambaye ninyi mnamwabudu bila kumjua* (22,23).'

Huu ni utalaamu mkuu sana. Paulo anawapongeza watu wa Athene kwa kuwa wao walikuwa watu wa dini. Na baadaye, anasema haya kwa uhakika, 'Niliona kwamba mojawapo wa miungu wenu alikuwa na maandiko ambayo yalimaanisha kwamba yupo mungu mmoja ambaye ninyi mwakiri kwamba hamjamjua bado. Huyu ndiye Mungu ambaye mimi nitamfahamisha kwenu ninyi kumhusu Yeye.'

Paulo anahubiri kwamba sote tu malimbuko ya Mungu ambaye aliyeumba mbingu na dunia. Hivyo basi, haiwezekani Mungu kuwa Yeye aliumbwa kwa dhahabu, fedha, mawe wala kwa miti. Yeye ananukuu baadhi ya watungaji mashairi wa Kiyunani, kwa kuwa hata mmoja wa watungaji

mashairi wao alikiri kwamba sisi tu malimbuko ya Mungu. Yeye anawanukulu wanafalsafa wao, na hapo mwishoni mwa ujumbe wake, anatangaza kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo. Wakati Paulo anapohubiri kuhusu kufufuka kwa wafu, baadhi ya walidhihaki, ilhali wengine walinena kuwa, 'tutakusikiliza wakati mwingine kuhusu jambo hili.' Hivyo basi, Paulo akawaondokea wao. Ingawa baadhi ya watu fulani waliungana naye kuamini, miongoni mwao alikuwa Dionisio Mwareopago, na mwanamke aitwaye Damari, na wengine pamoja nao (32-34).'

Wasomi wengi hawakubaliani kuhusu ujumbe wa Paulo katika mlima wa Mars. Baadhi yao wanaamini kwamba alishawishiwa na mvuto wa mila na desturi pale alipokuwa akinukulu watungaji mashairi pamoja na wana falsafa Wayunani, hivyo basi, mazao ya uinjilisti yalikuwa duni sana. Hakuna waraka wo wote kwa watu wa Athene kama ilivyo katika miji mingine kama Korintho na Efeso. Baadhi ya wana filosofia hawakubaliani na haya. Mimi mwenyewe nashawishika kwamba Paulo alikuzwa katika filosofia ya mahubiri ya uinjilisti kwa lile tukio la ushuhuda wake huko Athene.

## Injili Yaenda Korintho

Kutoka Athene, Paulo anasafiri moja kwa moja hadi Korintho. Korintho ulikuwa mji ambao ulikuwa umegumbikwa na dhambi kuu. Katika ulimwengu wa karne ya kwanza kumtaja 'Mkorintho' kulikuwa ni sawa na kusema mtu aliyekuwa hana nidhamu na ni mwovu. Paulo alipokuwa akifikiria kuhubiri Injili katika mji kama Korinto, alikuwa amejawa na hofu (1 Wakorintho 2:3). Bali, Mungu alimpa faraja kwa njia ya maono, '*Bwana akamwambia Paulo kwa maono usiku, Usiogope, bali nena, wala usinyamaze, kwa kuwa mimi ni pamoja nawe, wala hapana mtu atakayekushambulia ili kukudhuru; kwa maana mimi nina watu wengi katika mji huu* (Matendo 18:9,10).'

Paulo alikuwa na Pentekoste ya kibinafsi iliyomtayarisha kwa ajili ya huduma huko Korintho. Kuna vile tunaweza kusema kwamba alikuwa na ushuhuda ambao ulimtayarisha kwa ajili ya huduma yake huko Galatia, Efeso, Filipi na hata Korintho. Ujuzi huu ulikuwa ni usaidizi wa kiungu ambao ulimtia moyo kwa kweli ya Kristo aliyefufuka kuwa pamoja naye alipokuwa akieneza Injili katika miji iliyokuwa ya umuhimu mkuu katika mipangilio yake. Ishara na maajabu katika siku ya Pentekoste yaliendelea kama wimbi kutia nguvu kutibuliwa kwa kuitangaza Injili ya Yesu ambayo aliamuru Kanisa Lake kuhubiri. Mifumo ya Pentekoste iliipanda kanisa katika kizazi cha kwanza katika historia ya Kanisa.

Mtazamo ambao nimeshiriki nanyi kuhusu ujumbe wa Paulo aliohubiri huko Athene ni lazima ushirikishwe kwa mtizamo ambao anaushirikisha kwa waumini wa Korintho. Anawaandikia kwamba wakati alipotembea huko Korintho, alikuwa ameumua kutotumia 'maneno yenye kuvutia na yenye hekima yake mwanadamu,' ila kwamba kuhubiri kwa dhihirisho la Roho na nguvu (1 Wakorintho 2:1-5). Wakati Paulo alipohubiri ujumbe huo katika mlima wa Mars, alitumia maneno ya kuvutia na ya hekima ya mwanadamu.' Aliwanukuu malenga wa mashairi pamoja na wana falsafa na kufanya mahubiri yenye ushawishi.

Neno la Kiyunani ambalo maanake ni 'kuhubiri,' ni 'kufanya tangazo,' jinsi tangazo la mfalme lilivyowasilishwa kwa raia zake kwenye vijiji na kote mijini ya milki yake. Unaposoma mahubiri ya Paulo katika sura sita zinazotangulia katika kitabu hiki cha historia, tilia maanani kile Paulo alichojifunza huko Athene na Korintho kilikuwa ni msitari wa tariki katika mpangilio wa mfumo wake wa kuhubiri Injili.

Ninashawishika kwamba kati ya huduma zake huko Athene na Korintho, Paulo alikumbana na ushuhuda ambao ulishawishi mtazamo wake katika mpangilio wake wa kuhubiri Injili. Paulo alitambua kwamba kuhubiri ni huduma ya kiroho, na kile alichohitaji kufanya ni kutangaza kweli ya Injili kuhusu Yesu Kristo. Anamalizia waraka wake kwa Wakorintho kwa msemo mwingine kuhusu Injili aliyohubiri alipotembelea mji wao (15:1-4). Aliwaandikia Warumi kuwa: '*Mimi siionei haya Injili yake Yesu Kristo kwa kuwa hiyo <u>Injili</u> yenyewe, ndiyo nguvu zake Mungu kwake yule anayeamini* (Warumi 1:16).'

Baada ya Athene na Korintho, Paulo anatangaza ujumbe wa Injili na kwa mara nyingi awaeleza ushuhuda wake jinsi alivyoamini Injili hiyo.

### Paulo Akiwa Efeso

Huduma kuu ya Paulo alipokuwa mjini Efeso ilikuwa kutimiliza hamu yake kuu kufikia Asia kwa Injili. Huko Efeso, Paulo aliingia katika huduma yenye mazao mengi kwa kuazisha Kanisa. Wasomi wanaamini kwamba Kanisa lililoazishwa Efeso lilifanyika kuwa 'mama' ambalo kutoka kwake, Makanisa sita 'yalizaliwa,' ambayo yanatajwa katika Kitabu cha Ufunuo. Kanisa la Pergamo, Thiatira, Smirna, Filadelfia, Laodokia, na Sardi yawezekana kuwa yalikuwa Makanisa yaliyosimamiwa na lile la Efeso. Waraka wa Paulo kwa Wakolosai huenda ulikuwa umeelekezwa kwa Kanisa ambalo lilikuwa limezaliwa na lile la Efeso.

Sababu mmoja ya Kanisa lililoanzishwa huko Efeso kuwa lenye mazao mengi ni kwa sababu Paulo alikuwa na 'shule' huko. Tunasoma kwamba alikuwa akifunza katika '*chuo cha Tirano kwa muda wa miaka miwili* (Matendo 19:10).' Nakala moja ya kale linasema kwamba Paulo alikuwa na uwezo wa kuchukua na kufundisha katika chuo hiki tangu saa tano asubuhi hadi saa kumi na moja jioni kila siku wakati chuo hiki hakikuwa kikitumiwa. Katika eneo lile la ulimwengu, mchana hukatizwa kwa masaa kadha kwa usingizi wa adhuhuri hasa wakati kuna joto jingi hivi kwamba ni vigumu kufanya kazi au kuwa na darasa katika chuo kile.

Yawezekana kwamba Paulo alikuwa amewafunza wachungaji wa Makanisa haya katika chuo kile. Yamkini ni kwa sababu ya 'chuo' hiki Paulo akaishi kwa zaidi ya miaka mitatu kuliko alivyoishi kwenye miji mingine ambapo aliazisha Makanisa. Kanisa la Efeso lilikuwa limefunzwa vyema na huyu mchungaji mwalimu, kwenye nusu ya mwanzo katika waraka wake kwao, wakati mwingi akiwahimiza 'kukumbuka' kile alichokuwa amewafunza hapo awali.

Moja wapo ya ufunuo unaogusia kuhusu Paulo na huduma yake katika kitabu hiki cha historia unapatikana katika sura ya ishirini. Akiwa kwenye safari yake kuelekea Yerusalemu, ambapo Roho amemfahamisha kwamba atashikiwa, na kufungiwa hata kupigwa (Matendo 20:22-24). Alipofika mahali panapojulikana kama Melito, ambapo ni karibu na Efeso, alitambua kwamba hatakuwa karibu na waaminifu hao ambao alikuwa ameiweka raslimali kuu ya huduma yake kwao. Hivyo basi, alituma ujumbe wazee waje kwenye ufuo wa bahari wa Melito, na kuwaaga kwa mausia. Maneno ya Paulo ya mwisho kwa wazee hawa ni: *'Basi, sasa nawaweka katika mikono ya Mungu, na kwa neno la neema yake, ambalo laweza kuwajenga na kuwapa urithi pamoja nao wote waliotakaswa. Sikutamani fedha wala dhahabu, wala mavazi ya mtu. Ninyi wenyewe mnajua ya kuwa mikono yangu hii imetumika kwa mahitaji yangu na ya wale waliokuwa pamoja nami. Katika mambo yote nimewaonyesha ya kuwa kwa kushika kazi hivi imewapasa kuwasaidia wanyonge, na kuyakumbuka maneno ya Bwana, Jinsi alivyosema mwenyewe, Ni heri kutoa kuliko kupokea* (32-35).'

Kwa kuwa Paulo alikuwa akijitegemea mwenyewe huko Efeso, hakuna ye yote ambaye angeweza kumshtaki kwamba alihubiri na kufunza kwa kuwa alikuwa akitarajia dhawabu kutoka kwao. Kwa kweli, Paulo hakujitegemea mwenyewe tu, kwani pia alitimiza mahitaji ya kundi lile lililokuwa pamoja naye kwa kuwa aliwataka wao kujifunza ukweli wa maneno ya Yesu aliyosema hivi:

*'Ni baraka zaidi kutoa kuliko kupokea.'* Maneno hayo ya Yesu yanahitajika kuwa chanzo cha hamu yetu kufanya kazi kuu na ngumu. Ikiwa tutatenda kazi kwa juhudi na kupokea malipo yake, tutakuwa na kitu cha kutoa hivyo basi, tunaweza kujifunza 'sifa ya heri' ya tisa yake Yesu.

Wakati Paulo alipowaambia wazee hawa kuwa hawatapata kuona uso wake tena, *'walilia wote sana, wakamwangukia Paulo shingoni, wakambusu-busu.'* Huu ni ufunuo unaovutia sana kuhusu 'koinonia' au ushirika wa karibu ambao ulikuwepo hapo katika kizazi cha kwanza cha Kanisa.

## Sura Ya Nane
## 'Mitindo Ya Paulo'

Katika sura ya ishirini na moja, tunasoma kwamba Paulo aliwasili huko Yerusalemu na kuanza kuhubiri. Kama mapokezi kwa mahubiri yake, alivamiwa na kundi kubwa (27). Kwa hakika, walikuwa wamempiga Paulo kiasi ya kufa hadi alipookolewa na Jemedari wa kikosi cha Warumi aliyekuja na askari wengine na kumnyakua. Huku askari hawa wakiwa wamembeba Paulo juu juu hadi kwenye ngome ambapo angelikuwa mfungwa wa Kirumi, amsihi yule akida kumshusha chini na kumruhusu kuhubiri, kwa kuwa yeye aliona matukio haya kama fursa kuu ya kuhubiri. Alihubiri ujumbe mkuu, ambao unanakiliwa katika sura inayofuatia.

Huu si kama ule ujumbe wa mlimani Mars. Hapa, Paulo hakunukuu malenga wa mashairi wala wana filosofia au kutumia maneno matamu yenye kuvutia elimu ya mwanadamu. Alitoa ushuhuda wa mwenyewe katika Kristo Yesu. Nayo mapokezi ya watu yalihitilafiana. Tunasoma kuwa: 'Yale makutano yalimsikiza mpaka neno lile,' lakini wakapaza sauti yao wakisema, *'Mwondoe huyu katika nchi, kwa maana hafai aishi (22:22).'* Wakati hasira ya makutano haya inapowapanda, Paulo alipelekwa hadi ndani kwenye ngome.

Wakati Warumi walipomshika mtu fulani, ilikuwa desturi yao kumchukua na kumfungia kwenye mti na kumpiga mjeledi. Wao walitaja tabia hoyo kama 'kuhoji kwa mateso.' Na walipokuwa tayari kumfunga Paulo hili 'kumhoji,' aliwajulisha askari hao kwamba yeye ni raia wa Kirumi. Walipofahamishwa hayo, askari wale walimfahamisha yule jemedari wao asimpige (29). Kwa hakika, nashangaa ni kwa sababu gani Paulo na Sila hawakudai haki yao kama raia wa Kirumi walipopigwa na kufungiwa gerezani huko Filipi? Labda alijiruhusu mwenyewe kupigwa kwa sababu alikuwa akitaka kutumia fursa hiyo kwa wakuu wa mji.

Wakati Warumi walipoamua kwamba hawatampiga, walimfungia ndani ya gereza. Siku iliyofuatia, waliazimia kwamba wampeleka mahakamani ya makuhani na wakuu wa dini. Watu wa dini miongoni mwao walikuwa katika kundi lenye vurugu ambao walikuwa wamemshtaki Paulo walikaribishwa kuwasilisha mashtaka kinyume chake hapo mahakamani.

Nakala ya utaratibu wa mashtaka hatimaye ilimsalimisha Paulo kwa Kaisari kwenye sura ya ishirini na yatu. Tunaona utu wa kibinadamu wa Paulo wakati mashtaka yanawasilishwa kinyume chake. Anatazama kila upande na kutambua kuwa nusu ya wote waliofika mahakamani walikuwa Mafarisayo ilhali nusu ile nyingine ni Masadukayo. Mafarisayo walikuwa ni wale Wayahudi wafuasi wa desturi ya kale, ilhali Masadukayo walikuwa watu wenye desturi ya mabadiliko huru. Wale Masadukayo hawakuamini ufufuo wala mambo yasiyo ya kawaida. Hivyo basi, Paulo anawasilisha ujumbe mkuu kwenye baraza hili ile ambayo tayari ilikuwa na mgawanyiko wa mawazo. Alitangaza kwa heshima kuu: *'Ndugu zangu, mimi ni Farisayo, mwana wa Farisayo. Mimi nina hukumiwa kwa ajili ya tumaini la ufufuo wa wafu* (Matendo 23:6).'

Kwa maarifa mengi, wakati Paulo alipotangaza kuhusu ufufuo wa wafu, ubishi wenye mashindani baina ya Mafarisayo na Masadukayo ulizuka na mkutano ukafarakana, huku Mafarisayo wakiunga mkono msimamo wa Paulo. Paulo alifahamu kwamba alikuwa akishinikizwa kwenye mashtaka yasio haki, mashitaka yasio ya kweli. Hivyo basi, aliamua kuligeuza baraza lile upande wa juu chini jinsi alivyofanya kule Filipi. Iliwabidi askari kumwokoa kwa mara nyingine na kumpeleka hadi gerezani lililokuwa kwenye ngome kwa ajili ya usalama wake.

Arobaini kati ya Wayahudi hao walikutana wakafanya mapatano, wakajifunga kwa kiapo kwamba hawatakula wala hawatakunywa hata wamwue Paulo. Mpango wao ulikuwa kwamba wangevamia Paulo na kumwua wakati aliposhushwa huko kuhojiwa zaidi (12). Mpwaye Paulo alisikia habari za kuotea kwake za Wayahudi, hivyo basi akaenda akaingia ndani ya ngome akampasha Paulo habari. Kisha kijana huyo alimpasha Jemadari kile Wayahudi hao arobaini walichokuwa wakiotea kukifanya.

Yule Jemadari aliamua kumwondoa Paulo kutoka mikononi mwake. Yeye hakufahamu kile alichotenda wala shida walio kuwa nayo Wayahudi hao dhidi ya Paulo, ingawa alifahamu kwamba hakuna faida atakayopata kutokana na mtu huyo isipokuwa shida tu. Basi aliwaita maakida wawili na

kusema, '*Wekeni tayari askari mia mbili kwenda Kaisaria, na askari wapanda farasi sabini, na wenye mikuki mia mbili, kwa saa tatu ya usiku. Akawaambia kuweka wanyama tayari wampandishe Paulo, na kumchukua salama kwa Feliki liwali* (23, 24).'

Je! Tukio hili sio la kuvutia? Kwenye giza kuu, Myahudi mmoja na mdogo mwenye msimamo wa kibinafsi, akizungukwa na askari wa Kirumi mia nne na sabini, ambao walikuwa wakimtorosha kutoka gerezani lililokuwa kwenye ngome na kumsindikiza hadi ufuo wa bahari kuu la kati kutoka Yerusalemu hadi Kaisaria nchini Palestina.

## Mbele Za Liwali Wawili

Paulo alipowasili kule Kaisaria, aliwasilishwa kwa Liwali Feliki. Feliki aliwaamuru Wayahudi waje na kuwasilisha mashtaka rasmi dhidi ya Paulo kulingana na makosa yake. Hapa kwa mara nyingine, tuna ujumbe mwingine uliotolewa na mtume Paulo. Katika tukio hili, wakati Paulo alipohubiri mbele ya Liwali na kwenye mahakama hiyo, alielezea 'hadithi ya Mungu,' au ushuhuda wake.

Kulingana na maelezo ya Paulo, Feliki aliamua kwamba kwa hakika, hakuna sababu yake kushinikizwa kuwa amevunja sheria. Hata hivyo, aliamua kumweka Paulo chini ya usimamizi wake hadi atakapotoa uamuzi kuhusu kile kitakachotendeka kwa mfungwa huyo asiye wa kawaida (Matendo 24:22,23).

Liwali Feliki pamoja na mkewe Drusila ambaye ni Myahudi wamevutiwa sana na Paulo hivi kwamba wakamkaribisha kwa ajili ya kumsikiliza habari za imani iliyo kwa Yesu Kristo. Tunasoma kwamba Paulo ni mwenye furaha kutenda jambo hilo, lakini ujumbe wake ni wa kufedhehesha. *'Na Paulo alipokuwa akitoa hoja zake katika habari za haki, na kuwa na kiasi, na hukumu itakayokuja, Filiki akafanya hofu akajibu, Sasa enenda zako, nami nikipata nafasi nitakuita* (24, 25).'

Ni dhahiri kwamba huyu liwali alikuwa chini ya hukumu kuu ya Roho Mtakatifu aliposikiliza mahubiri ya Paulo, kwenye makutano ya watu wengi katika faragha. Alimkaribisha Paulo kwa wakati mwingi, lakini tunafahamishwa kwamba alitenda hivyo hili apate kupokea hogo kwa Paulo hili apate kumwachilia huru. Pia tunasoma kwamba alimweka Paulo gerezani hili akapate kibali kutoka kwa Wayahudi.

Baada ya miaka miwili, Feliki aliaga dunia naye liwali mwingine kwa jina Festo akachukua akatawala kwa niaba yake. Wakati huyu liwali Festo alipogundua kwamba alikuwa na mfungwa mwenye sifa nyingi za kidini na kisiasa kwenye mikono yake, aliamrisha afikishwe mbele ya mahakama hili kumhoji. Paulo anafahamu kwamba hatapokea haki ye yote katika mahakama yaliyo na ushawishi mwingi kutoka kwa Wayahudi walio huko Yerusalemu. Hivyo basi, alielezea nia yake kukata rufani mbele ya Kaisari ambayo ilikuwa ni haki yake kama raia wa Kirumi (Matendo 25:10). Yule liwali akasema, *'Wewe umeikata rufani kwake Kaisari. Na kwake Kaisari kwa hakika utakwenda!'*

## Mbele Ya Mfalme Agripa

Huku Paulo akingojea kusafiri hadi Roma, liwali Festo anatembelewa na mfalme – mfalme Agripa pamoja na malkia wake, Bernike. Baada ya kusikia habari za Paulo, wanasema kwamba wangependa kukutana naye (22). Kumbuka kwamba wakati Bwana alipomwambia Anania mpango Wake juu ya Paulo, Alisema, *'Yeye atalibeba jina langu kwa watu wa mataifa, wafalme na kwao wana wa Israeli* (Matendo 9:15).' Unabii huo unatimika wakati Paulo anapokutana na mfalme Agripa.

Baada ya kuletwa mbele za Agripa na Bernike, Paulo anatoa ujumbe mwingine wenye kuvutia sana. Kwa mara nyingine, aieleza hadithi yake na jinsi alivyookoka akiwa njiani kwenda Dameski. Paulo anapofikia mwisho wa ujumbe wake, yule liwali anafyatuka na kusema, *'Paulo, una wazimu, kusoma kwingi kumekugeuza akili* (Matendo 26:24).'

Usemi huu kwamba 'hauko peke yako' katika lugha ya Kiyunani ni, 'wewe ni mtu mwenye kujichagulia mambo yako mwenyewe,' au 'hauko shwari.' Kwa hakika, Paulo alikuwa mtu asiye wa kawaida. Alikuwa na kina kingine ambacho maisha yake yalikuwa yakizungukikia. Kina hicho kilikuwa ni Kristo ambaye alikutana naye njiani kuelekea Dameski. Sawa na Feliki, liwali Festo pia aligusiwa na maneno ya Paulo.

Paulo anamgeukia mfalme. Mfalme Agripa ni Myahudi, na hivyo Paulo anamwambia: *'Mfalme Agripa, Je! Wawaamini manabii? Najua ya kuwa wawaamini* (27). Agripa anamwambia Paulo, '*Kwa maneno machache, wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo* (28).'

Wasomi wa Biblia hawakubaliani ju ya maana ya mistari hii. Baadhi yao hawaamini kwamba huyu Agripa alikuwa akimaanisha kuhusu kufanyika Mkristo, ila kwamba usemi huo ulikuwa wenye

mzaha tu. Ninashawishika kwamba huyu Agripa alikuwa hafanyi mzaha, kwa kuwa mapokezi yake Paulo kutoka kwa Agripa yalikuwa ya kweli. Paulo anamjibu, '*Namwomba Mungu kwamba, ikiwa kwa machache au ikiwa kwa mengi, si wewe tu ila na hao wote wanaonisikia leo wawe kama mimi, isipokuwa vifungo hivi* (29).'

Sababu nyingine ambayo inanishawishi kwamba Agripa alikuwa wa kweli ni kwamba tunasoma kuhusu upokezi wake mfalme na malkia pamoja, naye yule liwali baada ya Paulo kusema: *'Mfalme na liwali na Bernike na wale walioketi pamoja nao wakasimama; hata walipoondoka wakasemezana, wakisema, Mtu huyu hatendi neno linalostahili kifo wala kufungwa. Agripa akamwambia Festo, Mtu huyo angeweza kufunguliwa, kama asingelitaka rufani kwa Kaisari* (30-32).'

## Safari Ya Paulo Huko Roma

Mojawapo ya hadhithi zenye kuvutia katika kitabu hiki cha historia ni nakala ya Luka kuhusu safari ya Paulo huko baharini kuelekea Roma (Matendo 27). Paulo alidhihirisha namna ya kipekee ya uongozi na kushuhudia miujiza kwa wale wote waliopona katika safari hii pamoja naye. Alipokea Neno kutoka kwa Bwana kwamba kwa sababu ya hali yenye kutisha ya anga, merikebu yao haingeweza kusafiri kuelekea Krete. Askari hao wa Kirumi hawakutaka kusikiliza maoni ya wafungwa.

Wakati dhoruba ambayo Paulo alitabiri ilipovuma, baada ya siku kumi na nne zenye dhoruba na tufani kuu, huku wakiwa hawawezi kula na wenye magonjwa kwa ajili ya kusafiri kwa merikebu baharini huku wakitapika na kulewa-lewa, Paulo aliwahubiria mabaharia waliokuwa wenye hofu manusurika (20-26). Paulo aliwahakikishia mabaharia hao kwamba Mungu alikuwa amemtokea na kumhakikishia kwamba ingawa merikebu yao ingeweza kuharibiwa, wote waliokuwa ndani wangenusurika.

Wakati neno hili la unabii ambalo lilipokewa na Paulo kutoka kwa Bwana lilipotimia, wale manusura walifika kwenye kisiwa cha Melita. Wanaota moto baada ya kuwa na ubaridi kwa siku nyingi baharini. Naye nyoka mwenye sumu kali alitoka kwenye kuni akamzonga-zonga Pualo mkononi. Wenyeji wa kisiwa kile waliamini kwamba Paulo alikuwa mwuaji,, ambaye ijapokuwa ameokoka katika bahari haki haimwachi kuishi. Lakini yeye alimtukusia motoni asipate madhara. Wao wakadhani ya kwamba atavimba au kuanguka chini kwa kufa ghafula; na wakiiisha

kumwangalia sana, na kuona kwamba halimpati dhara lo lote, wakageuka, wakasema kwamba ni mungu.

Wakati safari ya kwenda Roma ilipokifikia kikomo kupitia chombo kingine, Luka anaonyesha picha ya kuvutia ya jamii ya kiroho ambayo ni Kanisa la Kristo aliyefufuka huko Roma. Ni jambo la kugusia sana kusoma jinsi waumini huko Roma walivyokuwa tayari wamepashwa habari za kutarajiwa kwa Paulo, na jinsi alivyopata faraja na himizo moyoni mwake wakati waumini hawa walipokutana na mtume huyu akiingia katika mji huo akiwa kama mfungwa wa Roma.

Wakati wafungwa walipokuwa wakiletwa gerezani huko Roma, Paulo alipewa fursa kuishi katika nyumba ambayo alikodi na kuishi kama mfungwa wa nyumba kwa muda wa miaka miwili. Aliruhusiwa kukaribisha wakuu wa dini ya Kiyahudi huko Roma kwenye makao haya. Sambamba na ule mpango mwafaka wa Myahudi kwanza, alitangaza Injili pamoja na hoja yake kwamba Yesu ndiye Kristo. Baadhi ya waumini miongoni mwao wanabakia kuwa wenye chuki kinyume chake.

Katika makao yake ya kukodi, Paulo anaandika nyaraka zake zinazojulikana kama, ‘nyaraka kutoka gerezani’ – waraka kwa Wagalatia, Efeso, Filipi na Filemoni. Huku akiwa ameruhusiwa kutembelewa na wageni, fursa ya mwisho ambayo Luka anatuonyesha kuhusu mtume huyu mpendwa, alikuwa akihubiri habari za ufalme wa Mungu kwa kila mmoja aliyemtembelea na kumsikiliza (28:30,31).

*Isipokuwa kile tunachojifunza kutoka waraka wake kwa Timotheo, tunategemea historia ya Kanisa hili kufikia mwisho wa hadithi ya maisha pamoja na huduma yake. Wasomi wameshawishika kwamba Paulo alikuwa na mashtaka yake mahakamani mbele ya Kaisari, na kuwekwa huru, pamoja na kupewa msaada na Kanisa la Roma kueneza huduma yake ya umishonari hadi Uispania.*

Wakati Nero alipochoma mji wa Roma na kuwalaumu Wakristo, dhiki kuu iliyowakabili Wakristo na kudumu kwa muda wa karne tatu ilianzishwa kinyume cha Kanisa. Waumini wote walichukiwa na kuwa maadui wakuu wa serikali na watu wa Roma. Petro na Paulo walichukiwa zaidi ya wale wengine. Paulo alitiwa korokoroni mara nyingine. Wasomi wanashawishika kwamba alikuwa mfungwa katika gereza lile lililokuwa huko Mamertine, Roma ambako aliyaandika maneno yake ya mwisho kwa Timotheo kabla ya kukatwa kichwa.

Je! Umekutana na mtume huyu mkuu, mwenye kuvutia? Yeye ndiye mwandishi wa vitabu vifuatavyo kumi na vitatu katika Agano Jipya ambavyo tutachambua. Sote huwahitaji vinara vya watu wenye kuvutia kwa jinsi ya maisha au matendo yao ya imani. Maombi yangu ni kwamba utamkaribia na kumpenda Paulo jinsi nilivyofanya tangu niliposoma sura zilio katika kitabu cha Matendo ambazo tayari tumekagua.

Kote katika sura za mwisho za kitabu hiki cha historia, tuna shauku kwamba kilele cha safari ya Paulo kinatokea katika mji mkuu wa milki ya Warumi na katika mahakama mbele za Kaisari. Ni jambo la kushusha moyo ambalo halipendezi wakati kitabu hiki kinaposimama wala hakiendelei hadi mwisho. Wasomi wanashawishika kwamba inawezekana kwamba dhiki ndio sababu ya kitabu hiki kumalizika ghafula. Ukitizama sehemu ambazo ni za 'sisi', neno ambalo linazungumziwa badala ya kutaja majina katika sura mbili za mwisho inakuwa wazi kwamba Luka alikuwa pamoja na Paulo katika safari yake baharini wakati alipoingia katika mji wa Roma. Inawezekana kwamba Luka alikuwa ameshikwa na kufungwa hivi kwamba hangeweza kuendelea na kumaliza historia hii yenye kuvutia ya kizazi cha kwanza cha Kanisa.

Jinsi tulivyotazama hapo mwanzo wa kijitabu hiki chetu, inawezekana kwamba kulingana na mfumo wa Kiungu, historia hii ya Kanisa haikumalizika kwani sasa, tumekuwa tukiandika sura ya ishirini na tisa ya Matendo tangu Siku ya Pentekoste wakati Kanisa la Kristo lilipozaliwa.

## Ukaguzi Mfupi Wa Waraka Wa Paulo kwa Warumi

### Sura Ya Tisa
### 'Mtazamo Wa Juu Kwa Waraka Wa Paulo Kwa Warumi'

Mtume Paulo aliandika vitabu kumi na tatu kati ya ishirini na saba katika Agano Jipya. Kitabu cha kwanza ni waraka wake kwa Warumi. Paulo hakuandika nyaraka zake kulingana na mpangilio wake jinsi vinavyopatikana katika Agano Jipya. Wasomi wanaamini kwamba waraka huu uliandikwa mwishoni wa huduma yake, wakati alipokuwa amekomaa na tayari ameindeleza elimu ya thiolojia ya Injili ambayo alihubiri kote ulimwenguni ambayo anashiriki nasi katika waraka huu wenye uzito mkuu.

Hili kuwapa wasikilizaji wetu maelezo kuhusu vipindi vyetu sabini na saba kwenye redio ambazo ninafunza kotoka waraka wake Paulo kwa Warumi, msitari baada ya mwingine, tayari

nimeandika vitabu vingine vinne. Katika kitabu cha maoni kuhusu Warumi, ninaelezea baadhi ya nakala kutoka kwa wale ambao tayari wamesikiliza ukaguzi kwa muhtasari wa waraka huu wa Paulo. Kijitabu hiki ni ukaguzi mfupi wa yale Paulo anafundisha katika maelezo haya ya Injili anayotangaza.

Waraka wa Paulo kwa Warumi ni kipeo chake cha kithiolojia. Yaliyomo katika waraka huu yana mambo madogo sana yanayohusu Kanisa la Roma. Wasomi wanaamini kwamba Paulo anaelekeza waraka huu wenye maelezo sahihi kuhusu Injili kwa waumini wa Roma, kwa kuwa mji huo ulikuwa ndio mkuu ulimwenguni wakati alipoandika waraka huo.

Waraka huu kwa hakika ni maelezo sahihi ya neno la Kibiblia 'kufanywa haki.' Katika fumbo la Yesu kuhusu mtoza ushuru na Farisayo, anatangaza Habari Njema kwamba mtu ye yote au mwanamke ye yote yule ambaye atafanya maombi ya mwenye dhambi – maombi ya toba na kuamini katika nguvu za wokovu zipatikanazo katika kifo, mazishi na ufufuo wa Yesu Kristo kwa ajili ya dhambi zetu – anaweza kuelekea nyumbani akiwa 'amefanywa haki (Luke 18:14).' Hii ndio mara ya kwanza tunakutana na neno hili katika Agano Jipya. Katika waraka huu wake kwa Warumi, Paulo anaelezea jinsi Mungu hutenda muijiza wa kumfanya mtu haki ndani yake. Waraka huu ndio maelezo sahihi kuhusu jambo hili la kufanywa haki ambalo lipo katika Biblia.

Kufanywa haki kunamaanisha zaidi ya kusamehewa; kunamaanisha kwamba Mungu tayari amenifanya kana kwamba sijatenda dhambi hata kidogo, na kwamba amenitangaza kuwa haki. Kwa njia ya unabii, Daudi alidokeza jambo hili kuhusu dhana hii katika Zaburi yake ya kukiri na kutubu dhambi wakati anapomwomba Mungu 'kuondoa dhambi yake (Zaburi 51:1).'

Soma kitabu cha Warumi kwa wakati mmoja kisha ujaribu kutatuwa hoja kuu iliyopo. Ninakusihi kutenda hivi kwa kuwa waraka huu una hoja na somo linaloambatana kutoka mwanza hadi mwisho. Mwombe usaidizi Roho Mtakatifu na kwa hali ya utulivu, jaribu kutambuliza hoja kuu katika nakala hii ya Injili ya Yesu Kristo aliyowaamrisha wanafunzi kuhubiri kwa kila kiumbe na katika kila taifa ulimwenguni (Marko 16:15).

Sura za kwanza nne katika waraka huu zinaonyesha jinsi kufanywa haki kunavyohusiana na mwenye dhambi. Hatutapendezwa na kutangaza kuwa wenye haki hadi pale tutakaposhawishika kwamba tu wenye dhambi wasio haki. Hivyo basi, Paulo anawasilisha hoja yenye ushawishi mwingi kwamba sisi sote tu wenye dhambi. Baada ya kutushawishi kuhusu habari hii mbovu kuwa tu wenye

dhambi, Paulo anatangaza Habari Njema kwamba Mungu ana mpango ambao tunaweza kufanywa haki.

## Mpango Wa Mungu Kutufanya Haki

Kulingana na Paulo, neema ndio kina cha kufanywa haki (3:24). Msalaba wa Yesu Kristo ndio msingi wa kufanywa haki, nao ufufuo Wake ndio thamana ya pekee kuwa tumefanywa haki (3:25; 4:24, 25). Anamalizia hoja hii kwa maneno haya: *'Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu* Kristo (5:1).' Hivyo basi, imani ndio kanuni ambayo kwayo, sisi hutumia muijiza huu kwa dhambi zetu hivyo kuhesabiwa haki na Mungu. Hapo baadaye katika hoja yake, atatuambia kwamba Mungu ndiye Mwanzilishi wa kufanywa haki kwetu (8:33).'

Ninaweza kukufahamisha kwamba kuna kifurushi cha maneno ambacho kinapatikana mara mia moja na hamsini katika Biblia wakati dhana hii kuhusu kufanyika haki inapofunzwa. Maneno hayo ni 'katika machoni pake.' Kuwa mwelekeo na eneo la kwenda juu na upande unaohusika na kufanywa haki. Ikiwa tutakuwa tumefanya mauaji, tunaweza kuhesabiwa haki machoni pa Mungu kwa imani, na kwa kutubu, lakini hatufanywi huru kutoka gerezani kwa kuwa hatuko haki mbele za jamii, au upande wa wanadamu.

Wakati mashtaka yanapopelekwa mbele za hakimu bila baraza la washiriki kuwepo, wale wanaohudhuria mashtaka hayo wanaweza kudhani kwamba mshtakiwa huyo ni mtu mwema, ingawa hakimu huyo atafikiria kuwa ni mwenye hatia, na kwa hakika atampeleka gerezani au hata kupoteza maisha yake. Watu pia wanaweza kumfikiria kwamba mshtakiwa huyo ni mtu muovu, lakini hakimu huyo akiamini kwamba hana hatia, basi atamweka huru. Kwa njia ile ile, siku moja tutatambua kwamba cha maana zaidi ni kile Hakimu wa ulimwengu anachofikiria kama tuna au hatuna hatia. Hii ndiyo sababu kwamba ni Habari Njema kujulishwa kuwa tunaweza kufanywa-kana-kwamba hatujawahi kutenda dhambi mbele Zake.

Sura zinazofuatia nne zinanyesha jinsi kufanywa haki kunavyohusiana na mtu ambaye kwa hakika, amehesabiwa haki kwa imani. Mungu anatarajia kupata na kuwa haki, pamoja na kutenda haki wakati anapotutangaza kuwa wenye haki (1 Yohana 3:7). Katika sura nne zifuatazo katika waraka huu (5-8), Paulo anazungumzia kuhusu vita ambavyo vipo wakati ambapo mtu aliyehesabiwa haki anapogundua katika Roho Mtakatifu nguvu za kuishi maisha ya haki.

Katika sura tatu zifuatiazo (9-11), Paulo anaonyesha jinsi kufanywa haki kunavyoambatana na ulimwengu wote hasa kwa Israeli. Hizi ni mojawapo ya sura tatu zenye umuhimu mkuu katika Biblia katika somo la unabii. Ndani katika sura hizi tatu, Paulo anatabiri kwamba Israeli itahusika katika yale yanayoendelea ulimwenguni.

Kulingana na Paulo, Waisraeli ni watu waliochaguliwa wa Mungu. Wao ndio mfano mkuu katika Maandiko, hasa kuhusu mafunzo ya itikadi ya uchaguzi – kuhubiri kwamba Mungu huwachagua watu kwa ajili ya wokovu. Hata hivyo, katika sura hizi tatu, Paulo anaandika kwamba Wayahudi pia ni dhihirisho kuu katika Biblia kwamba Mungu amemuumba mtu kuwa kiumbe cha kujiamulia. Paulo anaeleza hivyo wakati anapotuambia kwamba Wayahudi wamechagua kutochaguliwa. Wao wamemkataa Yesu Kristo na wokovu.

Paulo anaandika kwamba, hili kuwarudi Wayahudi kwa kumkataa Masihi, Mungu amewageukia wale wa mataifa na amekuwa akiwaokoa tangu wakati walipomkataa Yesu Kristo. Wakati Mungu atakapokuwa amewaokoa watu wengi kutoka mataifa hili kuwaadhibu Israeli kikamilifu kwa ajili ya kumkataa Mungu, Atawarudia Wayahudi mara nyingine na 'Israeli yote itaokolewa (Warumi 11:26).'

Tumeshuhudia kutimizwa kwa unabii wa Agano la Kale kwamba kutakuwa na kurudi kwa Wayahudi katika eneo lao la Kijiografia kutoka kote walikotawanyika ulimwenguni na kuwa taifa la Israeli tena. Paulo anaungana na manabii wa Agano la Kale anapotabiri kurudi kwa Wayahudi kwake Mungu. Kurudi huko kwa kiroho bado hakujatokea. Katika sura hizi tatu, Paulo anaonyesha kwamba wakati watapoupokea ushuhuda huo wa kiroho na kumrudia Mungu, Atahusisha mpango wa kufanywa haki kwa ulimwengu wote kupitia Israeli.

Sura nne za mwisho (12-16) ni sehemu ya matimizo ya vitendo katika waraka huu wa kuvutia. Kila waraka wa Paulo umegawanyika kuwili. Kwanza, kuna sehemu ya mafunzo katika waraka huu, kisha sehemu ya matimizo kwa vitendo. Wakati wote tazama sehemu hii ya mafunzo na matimizo ya matendo katika nyaraka za Paulo.

Ingawa sura zile kumi na moja za kwanza katika waraka huu nni usemi na tangazo kuu la Injili ambalo Paulo aliliachia Kanisa, ilhali sura hizo nyingine tatu ni mojawapo ya zile ambazo ni

vigumu sana kuzielewa, hasa matangazo yake ya kithiolojia na unabii; sura nne za mwisho ni mojawapo ya zile ambazo matakwa na matimizo yake yaliyo dhahiri yanapatikana miongoni mwa nyaraka zake.

## Sura Ya Kumi

## 'Jinsi Ilivyokuwa – Jinsi ilivyo'

Sura ya kwanza ya waraka wa Paulo kwa Warumi ni sawa na sura ya kwanza katika kitabu cha Mwanzo. Maandiko ambayo huzungumzia mianzo hayatuambii jambo kuhusu jinsi ilivyokuwa bali kile Mungu anataka tuelewe jinsi kilivyo hata siku ya leo. Vile Paulo anavyomshirikisha mwenye dhambi katika dhana hii kuhusu kufanywa haki, baada ya kutuonyesha kama sote tu wenye dhambi, sehemu nyingine ni kwamba, sote tuko chini ya hukumu ya Mungu.

Anaendelea kutupatia uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu kama 'ulivyokuwa na jinsi ulivyo hata leo.' Mungu hubadilisha kile ambacho tunashikilia, au kule kuifinyila kweli iliyomo katika kutokuwa haki (Warumi 1:18). Anamaanisha kwamba wenye dhambi huazimia kuficha ukweli kwa sababu wanataka kutetea sera za maisha yao zisizo haki. Hawataki kuona ukweli kuhusu jinsi unavyohitajika kuishi maisha yao na kwamba Mungu anataka kujionyesha kwao. Yesu alifunza kanuni kwamba mtu akitaka kutenda, atafahamu (Yohana 7:17). Na kinyume chake pia ni kweli. Ikiwa hautaki kutenda, basi hautafamu kile Mungu anataka kutenda.

Mungu anatamka pia: *Kwa ajili ya hayo Mungu aliwaacha katika tamaa za mioyo yao, waufuate uchafu, hata wakavunjiana heshima miili yao. Hivyo Mungu aliwaacha wafuate tamaa zao za aibu, hata wanawake wakabadili matumizi ya asili kwa matumizi yasiyo ya asili; na kama walivyokataa kuwa na Mungu katika fahamu zao, Mungu aliwaacha wafuate akili zao zisizofaa, wayafanye yasiyowapasa.*

Hebu fikiria maisha yetu kama kitabu. Ni wazo la Mungu kuandika kitabu hiki naye ana mpango jinsi kinavyopaswa kuandikwa. Lakini anatupatia kalamu kwa wakati wake na kutuambia, 'hii, hapa kalamu, maliza hadithi hii jinsi upendavyo. Ni lazima uishi kwa matokeo yake, lakini unaweza kuandika hadithi hii jiinsi utakavyo.'

Tabia Ya Mwanadamu – Jinsi Ilivyokuwa – Jinsi Ilivyo

Paulo anaonyesha mambo ya kuvunja moyo kwa yale yatakayowatokea wanaoazimia kumaliza hadithi yao kwa njia hiyo. Anaandika kwamba wakati Mungu anapokata tamaa, wao hufanyika kuwa na ubatili akilini mwao, hali mioyo yao iliyo na upumbavu hutiwa giza. Kisha anamalizia kwa kueleza maisha yao kwa hivi: 'Yote hayana haki.' Huku akiwapa kibandiko kwa kutokuwa na haki, anatupatia mtazamo unaokubalika wa mwanadamu jinsi ulivyokuwa, na jinsi ulivyo siku ya leo (29-32). Orodha hii ndefu yenye kuhuzunisha dhambi inatuonyesha kile Isaya alichomaanisha wakati alipoandika kwamba sote kama kondoo tumepotea, na kila mmoja wetu ameigeukia njia yake (Isaya 53:6).

Tabia Ya Mungu – Jinsi Ilivyokuwa – Jinsi Ilivyo

Paulo kwa hakika, anaanza hoja hii katika waraka huu kwa kushiriki katika kutiwa nuru kulingana na tabia zetu. Anatoka kwa tabia ya mtu hadi ya Mungu wakati anapotuambia kwamba Mungu ni mwenye haki, na kwamba haki Yake pia hudhihirisha hukumu Yake kwa wale wasio haki (1:17). Kwa maelezo mengine, Mungu ndiye kipimo kamilifu kwa kile kinachokubalika na kuhitajika na Mungu kutoka kwa viumbe Wake wenye haki. Kwa hakika, Mungu anahukumu hali ya kutokuwa haki katika viumbe Vyake.

Aina mbili za tabia ya Mungu zinafunuliwa katika msitari huu muhimu: Haki pamoja na Hukumu ya Mungu. Hapa, Paulo anafanya hoja. Sisi tuna shaka kwa sababu ya tabia ya utu wa Mungu. Sisi sio wenye dhambi tu, bali tu wenye dhambi ambao wako chini ya hukumu. Tuna shida mbili ambazo hatuwezi kuzitatua. Habari Njema za waraka huu ni kwamba, Mungu tayari amezisuluhisha shida hizi mbili kwetu.

Baada ya Isaya kutangaza habari mbaya kwamba sote tumeigeukia njia yetu wenyewe, alihubiri tena Habari Njema kwamba '*Bwana alimuwekea juu yake uovu wetu sote* (Isaya 53:6).' Paulo alitenda jambo hilo hilo katika usemi wake wa Injili.

Hukumu ya Mungu inaweza kufafanuliwa kama 'tabia inayodumu, iliyo kinyume na kisicho takatifu,' au 'tabia inayodumu ya Mungu mwenye upendo kwa kile kinachoharibu chombo cha upendo Wake.' Maandiko yanatuambia kwamba upendo ndio utu halisi wa Mungu. Lakini wakati wale anaowapenda wamo katika hatari, karibu waharibiwe na dhambi, Mungu wetu mwenye upendo pia

ana uwezo wa hasira. Mungu huchukia na Mungu anahukumu dhambi kwa kuwa dhambi huharibu kile Anachopenda.

## Sura Ya Kumi Na Moja
## 'Wafalme Wanne Na Sheria Nne'

Paulo anamalizia hoja yake ya sura nne za kwanza katika msitari wa kwanza wa sura ya tano pale anapoandika: '*Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na tuwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.'* Huku akitujulisha sura nne katika sehemu ya pili ya hoja yake, anaendelea katika mstari ufuatao kwa kusema: *'ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo tunasimama ndani yake; na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu* (5:1,2).**'** Imani yetu katika msalaba wa Kristo inatufanya kuwa haki na kutupatia amani kwa Mungu. Imani pia hutupatia njia ya kwenda kwa neema ambayo hutuwezesha kusimama kwa ajili ya Kristo ulimwenguni, na kuishi maisha ambayo humtukuza Yesu na Mungu.

### Wafalme Wanne

Sasa kwa kuwa tumethibitishwa kuwa haki kwa imani, ni vipi ambavyo tumaishi kama watu ambao wametangazwa kuwa haki? Paulo anaanza jibu lake kwa swali hilo kwa funzo ambalo linaweza kutajwa kama *'Wafalme Wanne* (5:12-21).**'** Tunaweza kumtaja yule mfalme wa kwanza kuwa 'Mfalme Dhambi.' Tunasoma kwamba mfalme dhambi aliingia humu ulimwenguni na 'kuongezeka', au 'kutawanya wanadamu wote (12).**'** Paulo haingii katika majadiliano ya kifalsafa ya jinsi gani na kwa nini dhambi iliingia ulimwenguni. Yeye anaandika kwa urahisi kabisa kwamba dhambi iliingia, na kuongezeka, na kutawala.

Kifo nacho kikafuatia hapo baada ya mfalme Dhambi. Paulo anatuambia hapo baadaye kwamba, *'mshahara wa dhambi ni mauti* (6:23).**'** Dhambi wakati wote ina matokeo, nayo si mazuri. Mojawapo ya matokeo yale, ni mauti ya kawaida. Mauti pia ni fumbo ambalo humaanisha kwamba wakati wote ujira wa dhambi ni muovu. Punde si punde, sote tutaketi kwenye karamu ya matokeo. Wakati wote, mfalme Kifo hufuatana na mfalme Dhambi.

Wafalme hawa wawili wa kwanza ndio habari mbaya, lakini wafalme wawili wanaofuatia ni Habari Njema. Kulingana na Paulo, kuna mfalme wa tatu ambaye aliingia, na kuongezeka hata

kutawala katika maisha, naye ni Yesu Kristo. Mfalme Yesu alimshinda mfalme Dhambi juu ya msalaba, kisha baadaye akamshinda mfalme Kifo wakati alipofufuka katika wafu.

Tena Paulo ana Habari nyingine Njema. Mfalme wa nne ni Wewe. Kwa imani, unaweza kuingia katika uzima ndani ya Kristo. Unaweza kuongezeka katika Kristo kwa imani. Na wale ambao huingiza maisha katika Kristo na kupokea kwa neema na imani karama ya haki, 'atatawala katika maisha kupitia Yesu Kristo.' Kwa maelezo mengine, inawezekana kwako na kwangu kuingia kwa imani katika Kristo kwa njia ambayo tunaweza kutawala maisha kupitia Yeye (5:17). Yesu Kristo alisema, *'Nimekuja hili muwe nao uzima, na kisha muwe nao uzima tele* (Yohana 10:10).' Yamkini Paulo anatuambia jinsi ya kuingia katika uzima huu tele katika Kristo.

Wafalme hawa wanne ni Mashindi. Hatuwezi kuishi pamoja na dhambi hata jinsi ambavyo hatuwezi kuishi pamoja na maradhi ya saratani *(Cancer).* Dhambi itatushinda kwa kumtuma mfalme Dhambi. Lakini wakati kwa imani na neema tunapoingia katika uzima tele katika Kristo, tutakuwa tu washindi juu ya dhambi na kuwa na uzima tele. Wakati Paulo anapoifunga hoja hii yake katika sura ya nane, anatangaza kwamba tunaweza kuwa zaidi ya washindi wa dhambi na katika maisha (8:37)

## Sheria Nne

Fumbo la wafalme hawa wanne linaazisha hoja iliyopo katika sura nne kwenye sehemu ya pili katika waraka huu. Wafalme hawa wanne wanatutayarisha katika kusikia sheria nne za kiroho ambazo Paulo amaeleza katika sura mbili za mwisho kwenye sehemu ya pili ya waraka wake (5-8). Ikiwa tutakwenda kujifunza kuwa washindi ndani ya Kristo, ni lazima tujifunze sheria hizi nne za kiroho.

Sheria ya kwanza ni *'ya Mungu* (7:1-6).' Sheria ya Mungu ndio '*Neno Lake* (Zaburi 1:1,2).' Neno la Mungu ni muijiza mkuu. Imani huja kwa kusikia Neno la Mungu, nalo Neno hilo ndio mbegu isiyoharibika ambayo huzalisha maisha ya kiroho ndani mwetu (Warumi 10:17; 1 Petro 1:22, 23).

Sheria ya Mungu itatoa sheria ya pili ya kiroho ambayo ni 'Dhambi na Mauti.' Sheria hii ya pili ni timilifu, wala hakuna ubishi kwamba wakati wote, dhambi ina matokeo yake (7:7-25). Kulingana na Yakobo, Neno la Mungu ni kama kioo (Yakobo 1:23). Kazi ya kioo ni kutuonyesha upungufu uliopo katika utu wetu wa nje hili tukapate kujirekebisha kabla ya kutoka nje na kukutana na watu. Kwa njia hiyo, Neno la Mungu linatuonyesha dhambi iliyopo ndani ya maisha yetu hili tupate kushinda dhambi

yetu kabla ya kushirikiana na watu wengine. Ingawa si kitu cha kuvutia kila mara kutazama kioo, je! Ni wangapi miongoni mwetu ambao hukitupilia mbali nyumbani mwetu?

Na kama ilivyo kwa wale wafalme wanne, sheria mbili za kwanza hutangaza habari mbovu, na ya tatu na ya nne hutangaza Habari Njema. Paulo anataja sheria ya tatu ya kiroho kuwa '*sheria ya Roho wa Uzima katika Kristo* (8:1-4).' Anatuambia Habari Njema kwamba sheria hiii inaweza kutufanya huru kutokana na 'sheria ya Dhambi na Mauti.'

Jinsi sheria ya kupaa kwa ndege hushinda sheria ya uvutaji na kuiwezesha ndege kubwa ya abiria kupaa juu kutoka kwa uwanja, 'sheria ya Roho wa Uzima katika Kristo' ndiyo sheria ya 'kupaa kiroho' ambayo hutuwezesha kuinuliwa juu ya 'sheria ya Dhambi na Kifo.'

Kwa kuwa jambo hili ni kweli, ni kwa sababu gani wengi wetu hupoteza wakati wetu mwingi wa kiroho tukiwa kama marubani kwenye ndege ambayo ni ya Injini ambayo ina uwezo mkuu, huku tukibaki chini tu wala hatuwezi kupaa juu? Ingawa tumempokea Roho Mtakatifu, mbona hatuwezi kupaa na kushinda ile 'sheria ya Dhambi na Kifo?'

Jibu kwa Swali hilo linatutambulisha kwa sheria ya nne ya kiroho ambayo ni 'sheria ya Kiroho ya Mtizamo wa Nia.' Paulo anaandika kuwa: *'Kwa maana wale <u>wafuatao mwili ulio wa dhambi,</u> na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili; ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa <u>kufuata mambo ya mwili</u>, <u>bali mambo ya roho.</u> Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani. Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu* (8:5-8).' Ikiwa htuna ushindi juu ya sheria ya Dhambi na Mauti' maishani mwetu, ni kwa sababu *'tumeyaelekeza mawazo na nia zetu kwa mambo yaliyomo katika mwili.'*

Mojawapo ya mafunzo makuu ya Yesu yanaweza pia kutajwa kama 'sheria ya kiroho ya Mwelekeo na Nia ya Mawazo.' Yesu alifundisha kwamba tofauti kati ya maisha ambayo yamejawa na furaha na maisha yale ambayo yamejawa na kutokuwa na furaha ni jinsi sisi huyaona na kuyatazama mambo (Mathayo 6:22, 23). Viongozi wa kiroho, wana riadha, mabalozi na viongozi katika ulimwengu wa biashara wanathaminu sana mamno yao.

Kwa njia ya maombi, tilia maanani sheria hizi nne. Kisha ujiulize mwenyewe swali hili: 'Mtazamo wa mawazo yangu ni upi siku ya leo? 'Sheria ya mtazamo wa nia na mawazo' unaweza kuamua ikiwa 'sheria ya Roho ya Uzima ya Kristo,' au 'sheria ya Dhambi na Kifo' inatawala maisha yako.

## Sura Ya Kumi Na Mbili

## 'Mambo Yote'

*'Jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu! Hukumu zake hazichunguziki, wala njia zake hazitafutikani! Maana ni nani aliyeijua nia ya Bwana? Au ni nani aliyekuwa mshauri wake? Au ni nani aliyempa yeye kitu kwanza, naye atalipwa tena? Kwa kuwa <u>vitu</u> <u>vyote</u> vyatoka kwake, viko kwa uwezo wake, tena vinarejea kwake. Utukufu una yeye milele. Amina* (11:33-36).'

Hii ni zaburi ya kumsifu Mungu ambayo kwayo, Paulo anamalizia sehemu hii ya mafunzo haya makuu ya kithiolojia. Katika zaburi hii kuu ya sifa, Paulo anatangaza kwamba Mungu ndiye Shina la mambo yote, Nguvu iliopo nyuma mwa mambo yote, na kwamba utukufu wake ndio kusudi la mambo yote. Anatumia maneno haya mawili 'Vitu vyote' pamoja kwa mara nyingi, na si kwa tabia tu (Warumi 8:28; 2 Wakorintho 9:8). Je! Kwa hakika, ni mambo yapi ambayo Paulo anayagusia wakati anapoweka maneno hayo mawili pamoja katika wimbo huu wa sifa?

Tayari nimekushauri kugawanya sura hizi kumi na sita katika sehemu nne na kwa njia ya maombi, upambanie hoja kuu ya waraka huu. Sasa, ni lazima nikuulize kusahau kuhusu sura na mistari, huku ukijaribu kufahamu hoja hii iliyovuviwa katika waraka wa mtume Paulo kwenye waraka huu. Sura na mistari haikuwepo kwenye Biblia hadi karne ya kumi na tatu. Wakati mwingine, mgawanyiko huo wa sura unaweza kutupotosha kutokana na utaratibu wa hoja iliyovuviwa katika kitabu kwenye Biblia.

Paulo anaanza kujenga kuelekea kutumia maneno hayo mawili 'vitu vyote' katika wimbo huu wa sifa anapofika mwisho katika kutueleza kuhusu zile sheria nne za kiroho (8:13). Baadaye, anatupatia mtazamo wote jinsi Mungu alivyoleta wokovu. Lengo lake ni kwamba, Mungu ndiye Mwanzilishi Mkuu wa kila kitu ambacho hutendeka kwetu katika utaratibu wa kuokolewa. Anaandika hivi: *'Maana wale <u>aliowajua tangu asili</u>, <u>aliwachagua tangu asili</u> wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi. Na wale aliowachagua tangu asili.*

*Hao akawaita; na wale aliowaita, hao akawahesabia haki; na wale aliowahesabia hake, hao akawatukuza* (Warumi 8:29,30).'

Kifungu hiki kinaandaa wimbo wa sifa ulio mkuu wa kipekee. Mtume anatangaza kwamba Mungu yumo ndani mwa wale waliompokea. Yeye yupo pamoja na wale wanaotembea katika utiifu Naye. Ni wale walioitwa kulingana na Mapenzi Yake. Wakati Mungu yumo ndani na pamoja nasi, na pia kwa ajili yetu, ni nani awezaye kuwa kinyume chetu, na ni kipi ambacho kinaweza kututenganisha na upendo Wake? Yeye anamalizia sura hii ya nane kwa wimbo wa sifa kuu ambao unajibu maswali hayo.

Yachukue mawazo haya yaliyovuviwa pamoja nawe hadi kwenye sura ya tisa ambapo mtume anafafanua maneno haya anayoyatumia katika kifungu kilichotangulia. Maneno haya kuhusu 'kuchagua tangu asili.' Ufananuzi wa Paulo kuhusu dhana hii ambayo inafahamika kama 'Uchaguzi tangu asili' unaifanya kuwa moja ya sura za ibada zilizo ngumu katika Biblia.

Mfano wake katika dhana hii ni mapacha – Esau na Yakobo – wakiwa tumboni mwa mama yao. Kabla ya kutenda cho chote kizuri au kibaya, Mungu asema, *'Yakobo nampenda, bali namchukia Esau,'* na '*aliye mkubwa atamtumikia yeye aliye mdogo* (9:12,13).**'** Mungu ana lengo la baadaye, mpango kwa hawa mapacha wawili hata kabla yao kuzaliwa.

Mmoja wa wasomi nimpendao alisema kwamba funzo hili linahitajika kuwekwa kama siri ya kijamii kati ya waumini. Hatuhitajiki kuwatarajia wale ambao bado hawajajiunga na imani na kumpokea Roho Mtakatifu, kuelewa na kukubaliana na funzo hili. Ni vigumu zaidi kwa waumini wengi kwa sababu humfanya Mungu kuonekana kama ni mwenye kupendelea, hasa kwa wale ambao 'hawajachaguliwa.'

Wakati mwingi, waumini kwa mara ya kwanza wanapovumbua funzo hili katika Maandiko, wao husema kwamba jambo kama hili haliwezekani kamwe wala si la kweli. Jibu la mtume kwa wazo hilo ni kutupa changa moto hili kusoma Agano la Kale. Moja ya mashairi mafupi kabisa ambalo nishawahi kulisikia ni hili: 'Ajabu gani – kwake Mungu – kuwachagua – Wayahudi.'

Kuna mwelekeo fulani ambao kwa ajili ya Agano la Kale, lote ni mfano wa funzo hili kuhusu uchaguzi. Kati ya mataifa yote ya historia ya kale, Mungu alichagua Israeli. Jinsi nilivyoonyesha hapo

mwanzoni, sura hizi tatu ni ngumu sana (9-11). Pia, zinaonyesha kinyume cha uchaguzi, kwa kuwa Israeli ilichagua – na inaendelea kuchagua hata siku ya leo – kutoteuliwa.

Mungu anatuambia kupitia Isaya kwamba tusijaribu kuelewa mawazo Yake wala Njia Zake. Anatuonya kwamba njia zake za mawazo na kutenda ni tofauti na zetu jinsi mbingu zilivyo juu kuliko nchi (Isaya 55:8,9).

Anapotoa mafunzo yake, Paulo anatoa changa moto kwetu kwa njia ya maswali haya makuu: *'Wewe ni nani, mwanadamu kumwuliza Mungu kwa nini umeumba Musa na Farao kutoka kwa udongo mmoja? Je! Udongo unaweza kumwambia mfinyanzi jinsi utakavyoundwa?* (9:20, 21).' Pia, anatoa maelezo kwamba uchaguzi sio jambo kuu wala la msingi. Ikwa tumechaguliwa kwa ajili ya wokovu, jambo lililo muhimu ni kwamba, tumeokolewa kwa neema wala sio kwa matendo yatokanayo na juhudi zetu wenyewe (11).

Wimbo wa sifa ambao tulianza sura hii nao pamoja na Paulo unamalizia kwa tamshi kuhusu itikadi katika thiolojia hii kuu na ndio njia ya kipekee ambayo tunaweza kupokea kila kitu ambacho Paulo alishiriki pamoja nasi, pamoja na funzo hili kuhusu uchaguzi. Paulo anatukumbusha katika wimbo huu wa sifa kwamba Mungu hakuhitaji ye yote miongoni mwetu awe mshauri wake wakati alipokuwa akitenda yote ambayo Paulo alikuwa nayo mawazoni mwake anapotuambia kwamba Mungu ndiye shina la, nguvu zilizomo nyuma, na kusudi la mambo yote.

## Sura Ya Kumi Na Tatu
## 'Hivyo Basi?'

Sasa, zoa kweli kutoka kwa wimbo huu wa sifa pamoja nawe hadi katika sura ya kumi na mbili. Wakati Paulo anapotumia neno, 'hivyo basi' twahitajika wakati wote kujiuliza ni kwa sababu gani maneno yale yamo pale.' Shauri hilo lenye hekima niliyopata yamkini miaka hamsini iliyopita linatusaidia katika kuifuata hoja ya mtume kwa utaratibu. Hii ndio njia ambayo wakati mwingi, yeye huanza sehemu ya utekelezaji katika nyaraka zake. Anapoanza kutekeleza kweli ambayo ameishiriki pamoja nasi katika waraka huu, matumizi yake ya maneno haya, lengo lake ni kutuelekeza hadi mwanzo mwa hoja yake (1:17).

*'Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya*

*dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu (Warumi* 12:1, 2).'

Watu wengi wanaamini kwamba ikiwa watajitolea kwa Mungu, mapenzi Yake yatawaongoza mahali paovu ambapo waweza kuwazia. Lakini Paulo anatuambia kwamba mapenzi ya Mungu ni ya kupendeza. Kwa kweli, ni makamilifu (2). Je! Wawezaji kufahamu mapenzi ya Mungu kwa maisha yako? Paulo anatupa hatua tano kwa mapenzi ya Mungu.

Kwanza, mfanye Mungu kuwa kina chako. Kwa kuwa Mungu ndiye shina la mambo yote, nguvu zilizo nyuma ya mambo yote, na kusudi la mambo yote, ni jambo linalokubalika kumfanya Mungu kuwa shina la maisha yako.

La Pili, jitolee kwa Mungu. Ni lazima tujitolee kwa kutoa mapenzi yetu kwa mapenzi ya Mungu. Kumbuka kanuni ambayo Yesu alitupatia wakati aliposema, '*Ikiwa mtu ye yote atayafanya mapenzi ya Mungu, yeye atafahamu* (Yohana 7:17).' Ikiwa Mungu anafahamu kwamba umejitolea Kwake, nawe unataka kutenda mapenzi Yake, atakuonyesha mapenzi Yake kwa maisha yako.

Hatua ya tatu ni ile ambayo wajitolea bila kutenda lo lote. Paulo anatuambia tuokolewe na Mungu*. 'Mbadilishwe kwa kufanywa upya katika nia zenu.'* Ulipozaliwa katika mwili, haukulitenda lo lote, lilikuwa tukio ambalo haukuchangia lo lote. Hii pia ni kweli wakati tunazaliwa kwa mara ya pili. Mungu ndiye hutushughulikia hali sisi huwa tunafanywa upya katika nia zetu (2 Wakoritho 3:18; 5:17,18). Tunaposhuhudia 'kufanywa upya katika nia zetu,' huwa tunaweza kuthibitisha kwamba mpango wa Mungu kwa ajili yetu ni mwema, na unatimiza masharti yake yote na kutusogeza kuelekea kukomaa kiroho.

Paulo anatutakia hatua ya nne wakati anapoandika: '*Msifananishwe na ulimwengu huu* (2).' Kwa maelezo mengine, *'Usifananishwe na mtu mwingie. Usiruhusu ulimwengu kukufinya kwa mfumo wake.'* Ukifanya hivyo, utapoteza mapenzi ya Mungu kwa maisha yako. Ikiwa wewe utafananishwa, Yesu Kristo atakufanya kuwa mtu asiyeambatana na mambo ya ulimwengu. Thamani zako hazitaambatana na thamani za watu wa ulimwengu ambao wanakuzunguka.

Mwisho, hatua ya tano ni kufanyika katika Kristo. Kulingana na Paulo, njia moja ya kutenda hivyo ni kutambua kwamba Roho Mtakatifu hutenda kazi kupitia watu wake kupitia karama za kiroho

(3-8). Karama hizi huthibitisha maisha yetu katika Kristo na kutuwezesha kutenda kazo zetu za kiroho. Tunapogundua ni kipawa kipi ambacho Mungu ameweka raslimali ndani yetu, na kujitolea kutenda yatakikanayo katika vipawa hivyo kwa ajili Yake, vipawa hivyo vya kiroho vitatuongoza katika mapenzi ya Mungu na kusudi katika maisha haya ya kuokolewa (Waefeso 2:10).

Kuwa Kweli

Huku Paulo akiendelea katika utekelezaji wake, anatushauri kuushirikisha ukweli wote ambao tumeshiriki naye katika waraka huu kwa kusanyiko la Kanisani ambalo tu sehemu yake. Tafsiri niipendayo ya Agano Jipya inatumia neno 'kweli' kote katika sehemu ya utekelezaji katika waraka huu. Kwanza, anaandika: *'Kichukie kile kilicho kiovu. Kishikilie kilicho chema* (9).' Mahali hapa, anatutia usafi na utakatifu miongoni mwa waumini.

Paulo pia anatupatia mwito wa unyenyekevu wa kweli: '*Usiyaweke mawazo yako kwa mambo ya juu, ila shirikiana nao wale wanyenyekevu* (16).' Unyenyekevu ni wema ambao wakati wote uko juu katika orodha ya matakwa ya mitume. Kisha anatupatia mwito wa umoja wa kweli. Umoja ambao Paulo anatangaza mahali hapa misingi yake imo katika kweli kwamba sote tu kitu kimoja katika Kristo na tu washiriki wa mwili Wake.

Wakati Paulo anapoandika, 'Mjitolee mtu kwa mwenzake katika hali ya upendo wa kindugu,' anamaanisha kwamba twahitaji kuwa na upendo wa kweli kwa wenzetu. Anapotoa maelezo kuhusu upendo ambao atuelezea katika waraka wake kwa Wakorintho, atatuonyesha kweli muhimu ambayo imo katika sehemu ya utendaji katika nyaraka zote zake.

Kisha Paulo anatoa mwito wa utumishi wa kweli. *'Shiriki na watu wa Mungu walio na mahitaji* (13).' Paulo anautaja ukarimu kama moja ya karama za kiroho. Kwa lugha ya asili, Paulo anafunza kwamba si jambo la kawaida kwetu kujitolea kwa ukarimu, ila sisi 'huwapa watu dhiki' kwa upendo. Pahala pawili Paulo anapotoa mwongozo kuhusu matumizi ya watumishi waaminifu kwa Kanisa ni: kuenezwa kwa Injili pamoja na mahitaji ya waumini.

Paulo anatoa mwito kwa matendo yaliyo ya kweli. Fursa ya matendo haiwezi kuchukuliwa na ile ya uzalishaji. Paulo anaandika*: Msiwe wavivu katika kutenda kazi, mwe na moyo mkuu, katika kumtumikia Bwana.'* Neno 'kazi' hapa kwa hakika ni 'kule kuitenda kazi.' Kwa hakika, Paulo anatupa changa moto tuwe na thamani za kweli. Kwa kuhusika katika mambo mengi, ye yote kati yetu

atakuwa na hatia ya kuongozwa na 'utawala wa kimabavu kutoka kwa mambo yasiyo muhimu ila yanayohitajika kwa haraka.' Hatuchukui wakati wa maombi kuelekeza vyema thamani zetu.

Mtume Paulo alikuwa mtu ambaye alifahamu thamani zake. Angeandika*: 'kitu kimoja mimi na kitenda (*Wafilipi 3:13).' Tambua vile watu wamchao Mungu ambao tunawasoma katika Biblia wanavyoungana na Paulo katika nidhamu hii ya kiroho ya kutilia mkazo thamani zao. Daudi aliandika: *'Neno moja nimelitaka kwa Bwana, Nalo ndilo nitakalolitafuta* (Zaburi 27:4).' Neno hili moja ambayo Daudi na Paulo walichukulia kuwa ya thamani ilikuwa ni uhusiano wao na Mungu na katika kuthibiti mapenzi Yake kwao kwa ushuhuda wa kila siku. Hamna mfano mwingine bora kuhusu nidhamu ya kutilia thamani umuhimu katika Biblia kuliko vile Yesu Kristo alivyotekeleza thamani zake.

Paulo anazidi kuwahimiza wanaoamini ukweli wa Injili ambayo ameishiriki pamoja nasi kuwa na hamu ya kweli, ushuhuda, maombi pamoja na imani (14-21). Kwa mara nyingine hebu tazama mkazo wa kila siku katika utekelezaji wa kweli ya Injili katika maisha yetu kwenye sura za utekelezaji wa elimu hii ya kithiolojia tunaita 'waraka wa Paulo kwa Warumi.'

## Waumini Kama Raia

Katika sura ya kumi na tatu, Paulo anatuonyesha jinsi ya kutumia Injili ya kufanywa haki kwa imani kama raia. Ingawa jinsi tumejifunza katika kitabu cha Matendo, kuna wakati wa mwaminifu uasi au kutoitii serikali wakati zake ni kinyume na mafunzo ya Mungu. Katika sura hii, Paulo aandika mara tatu kwamba wakuu wa serikali ambao hutunza na kulinda sheria ni '*mtumishi wa Mungu (*13:4,6).' Kama mtumishi wa Mungu aliyechaguliwa, ni kielelezo cha Mungu kuhusu hasira Yake (4).

Paulo hazungumzii kuhusu watunza sheria waliozaliwa kwa mara ya pili, ila wale askari wa Kirumi. Neno 'kuchaguliwa' lina maana 'kuwekwa mahala mwafaka.' Watumishi wa Injili walio wekwa wakfu kwa kazi fulani *(ordained)* au kuchaguliwa huwa wamewekwa mahali mwafaka hili kuhubiri sheria ya Mungu. Askari waliochaguliwa kutunza amani huwa wamechaguliwa hili kutunza sheria ya Mungu. Paulo anasema, 'ikiwa unataka kuambatana nao, basi tunza sheria. Lakini ukihusika katika wizi au mauaji, nao watatutumia upanga juu yako, na wanapofanya hivyo, wanakuwa watumishi wa Mungu.'

Kwa sababu dhana hii kwamba kunahitajika kuwa na sheria na utangamano inatoka kwa Mungu, vivi ndivyo yule afisa mtunza sheria anavyovumbua kwamba mwanzo wa mamlaka yake ni

Mungu. Hata hivyo, wakati serikali imekumbwa na ufisadi na uchafu mwingi, na sheria zake zinapingana naza Mungu, kuna uwezekano wa kuasi serikali (Matendo 5:29).

## Ubishi Wa Wanafunzi

Katika sura ya kumi na nne, Paulo anaelekeza matematumizi yake kwa ubishi miongoni mwa wanafunzi waliomo Roma. Paulo hakuwa amewatembelea wanafunzi hawa huko Roma, lakini kwa kuwa njia zote zilielekea huko Roma wakati alipoandika waraka huu, aliwafahamu waumini wengi waliokuwa wemetembea huko au wale ambao hapo baadaye wangesafiri hadi humo. Yeye alifahamu kwamba kulikuwepo ubishi huko.

Kongamano kuu la kwanza la Baraza la Kanisa lilifanyika hili kulitatua jambo hili: Wanafunzi wa Yesu wa kimataifa hawakutaka kuishi kama Wayahudi wenye juhudi kuu, ilhali Wayahudi waliokuwa wamezaliwa mara ya pili walikuwa wakitaka kuzidi na kuishi kulingana na desturi zao za kidini kwa kuwa walikuwa wakimfuata Masihi wa Kiyahudi (Matendo 15). Kongamano hilo kuu la Baraza la Kanisa liliafikiana kuwa wanafunzi wa kimataifa hawahitajika kuwa kama Wayahudi, ilhali wanafunzi wa Kiyahudi waliruhusiwa kuishi kulingana na desturi zao. Huku makundi yote mawili yakizidi kumfuata Kristo, pia walizidi kuwa na tofauti kuu –hasa kuhusu itikadi za vyakula na sherehe kuhusu siku kuu zao Wayahudi.

*Baadhi ya waumini wa Kiyahudi waliendelea kusheherekea siku ya Sabato (Saba) kama siku ambayo imetengwa kwa ajili ya Mungu kwa ibada, mapumziko na uhuishaji. Hili kusheherekea ufufuo wa Yesu, mitume ambao walikuwa Wayahudi walibadilisha siku yao ya ibada kutoka ile ya saba hadi ya kwanza ya juma. Watu wa mataifa waliozaliwa kwa mara ya pili hawakuelewa sababu ya kutenga kando siku ya saba kwa ajili ya ibada.*

Paulo aliwashauri waumini hao Wakirumi kutatua ubishi huo wao kulingana na msingi huu: *'Mtu mmoja afanya tofauti kati ya siku na siku, mwingine aona siku zote kuwa sawa. Kila mtu na athibitike katika akili zake mwenyewe* (14:5) Anamaanisha kwamba baadhi ya waumini walichukulia kila siku ya juma kuwa siku ya Bwana.

Je! Maana ya 'kushawishika kikamilifu' ni nini katika kujadili mabishano haya? Kwanza, Paulo anaandika kwamba tunahitaji kushawishika kikamilifu kulingana na dhamiri yetu. Mtu fulani alisema hivi: 'Dhamiri ni sauti ile tulivu na nyororo ambayo hutufanya kujihisi kuwa wadogo zaidi.'

Sehemu kuu ya dhamira zetu ni itiko letu kwa yale yote ambayo tumefunzwa na wazazi wetu pamoja na watu wengine kwa miaka mingi.

Ni jambo la muhimu kutambua kwamba Paulo hasemi wala kuhimiza kwamba dhamiri ina usalama wa kuaminika kikamilifu. Lakini anatushauri kusikiliza dhamira yetu wakati inatueleza ikiwa jambo lile tunalotenda ni mbovu. Anathibitisha mapatano yale yaliyoafikiwa kwenye kongamano la kwanza la Baraza kuu la Kanisa kwamba waumini wa Kiyahudi walikuwa na haki na wajibu kuheshimu desturi yao ya vyakula na siku kuu zao za kidini, ilhali waumini wa kimataifa wasilazimishwe kufanyika Wayahudi katika mambo hayo.

Paulo anasonga hatua nyingine zaidi wakati anapoandika kwamba unahitaji kushawishika kabisa katika nia na akili zako kulingana na kusadiki kwako mwenyewe (6). Kusadiki hakutegemei malezi yetu kutoka kwa wazazi wetu. Ni matokeo ya kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha yetu. Roho Mtakatifu huwashawishi waumini wote kwa njia moja tu.

Paulo anaendelea mbele na kusema kwamba tunahitaji kusuluhisha mambo hayo kulingana na 'utambuzi' wetu kwa ndugu ambao hutofautiana nasi (10-23). Hata kama huyu ndugu hana haki kufanya hivyo, ikiwa yeye anaamini kwa dhamiri na kusadiki kwamba kuna kitu kibaya, sisi tunawajibika kwake. Anaorodhesha kanuni hii kwa upana katika (1 Wakorintho 8-10). Anawaandikia Warumi na Wakorintho kwamba jambo lililo hapa sio lile linalokubalika au lile lisilokubalika, ila ni kiwango kile tunampenda ndugu yetu. Hatuhitajiki kumkwaza ndugu yetu, bali tunafaa kufanya cho chote tuwezacho hili kumjenga. Mwisho, Paulo anatuhimiza tusuluhishe mabishano yetu kwa msingi wa upendo ambao anaorodhesha katika sura yake ya Upendo (Wakorintho 13).

## Moyo Wa Umishionari Wa Paulo

Kwa hakika, tunamfahamu mtume Paulo katika sura ya kumi na tano. Ulimwengu ulikuwa katika moyo wa mtume huyu. Katika kitabu cha Matendo, tulimwona Paulo akiwa na shauku kuu kuhusu Roma. Hata hivyo, wakati huu Paulo anawaandikia Warumi, *'nitakapokuwa nikisafiri hadi Uispania, nitakuja kwenu. Kwa kuwa ninatumainia kwamba nitawaona ninyi katika safari yangu na kupata msaada wenu njiani kuelekea kule* (24).' Maono yake yanaenda mbele ya Roma. Anashaka katika kusafiri hadi Roma kwa kuwa anatarajia waumini Warumi wampatie usaidizi muhimu hili apate kuhubiri Injili huko Uispania.

Matumizi Ya Kibinafsi

Hatuwezi kuepuka changa moto ambalo tunaliona kwa mtume Paulo akitekeleza ulimwenguni kote Injili aliyoieleza kwa ufasaha katika waraka huu. Tunapomalizia ukaguzi huu wa waraka wa Paulo kwa Warumi, changa moto iliyo dhahiri ni kwako wewe na mimi kwanza kutekeleza kweli iliyopo katika waraka huu kibinafsi. Je! Tuna amani kwa Mungu kupitia imani yetu ya kibinafsi katika yale Yesu Kristo aliyotenda kwa ajili yetu juu ya msalaba? Je! Tumepata fursa yetu ya kibinafsi kwa imani katika neema ambayo hutuwezesha kusimama kwa ajili ya Kristo ulimwenguni na kuishi kama mtu aliyehesabiwa haki na Mungu – maisha ambayo humtukuza Mungu? Je! Wewe unatawala katika maisha kwa imani ya Mfalme wetu Yesu? Je! Tumeweka mawazo yetu juu ya 'sheria ya Roho ya Uzima katika Kristo' ambayo inatuweka huru dhidi ya 'sheria ya Dhambi na Mauti?

Hivyo basi, ni lazima tutekeleze kweli ya waraka huu kwa ndugu katika ushirika wetu Kanisani, katika hali ya kiraia yetu na uhusiano wetu na serikali. Mwishowe, kama huyu mtume mpendwa, ni lazima tutekeleze kweli hii kuu ya kithiolojia kwa wale waliopo katika ulimwengu wetu wa leo ambao bado hawajasikia Injili hii yetu utukufu. Chambilecho Paulo, sisi tu wadeni kwa wale wote watuzungukao na tunahitajika kuwa tayari kuhubiri na kuishiriki Habari Njema ya Kristo bila kuwa na aibu: Kwa kuwa ni nguvu za Mungu hadi wokovu kwa kila mtu anayeamini
(Warumi 1:14-16).